# MADA: MTINDO KATIKA *ARUSI YA BULDOZA NA HADITHI NYINGINE*

NA

SAMSON ONTIRI ONGARORA

University of NAIROBI Library
0496787 3

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA "MASTER OF ARTS" KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

JUNI, 2007

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine cho chote.

..........................................................

Samson Ontiri Ongarora

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii walioteuliwa na Chuo Kikuu.

..........................................................

Dkt. A. M. Mbatiah

(Msimamizi)

..........................................................

Dkt. E. M. Mbuthia

(Msimamizi)

## TABARUKU

Kwa wazazi wangu: Peter Ongarora na Keziah Moraa walionilea na kunielimisha.

# SHUKRANI

Ningependa kumshukuru Mungu kwa kunipa siha njema tangu nilipozaliwa na kuniwezesha kukwea ngazi za elimu hadi kiwango hiki cha uzamili. Aidha, shukrani za pekee ni kwa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kufadhili masomo yangu ya uzamili.

Ninawashukuru sana wasimamizi wangu Dkt. A. M. Mbatiah na Dkt. E.M. Mbuthia kwa mwongozo na ushauri mwafaka walionipatia katika kuandika tasnifu hii. Mbali na hao, ninawashehenezea shukrani jazila wahadhiri wafuatao kwa mihadhara yao iliyonipa msingi thabiti wa kubobea katika Kiswahili: Profesa Mohamed Abdulaziz, Dkt. Rayya Timammy, Dkt. K. Wamitila, Dkt. John Habwe, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Tom Olali, mwalimu Iribe Mwangi, Ayub Mukhwana, Amir Swaleh na B. Mungania.

Sitawasahau wanafunzi wenzangu tuliosaidiana nao si kwa vitabu, si mijadala na kutiana shime maji yalipozidi unga. Hawa ni: Enock Matundura, Gerald Mogere, Henry Njoroge, John Mutua, Gabriel Kioni na Evans Ogoro.

Kwa ndugu zangu Isaac, Joash, Haron, Isaiah, Ben na dada Ann, Stella na Everline, ahsanteni kwa mchango wenu wa dua na uvumilivu nilipokuwa mbali nanyi. Aidha, nawashukuru mno Irene Moraa, Jackline na Ruth kwa msaada wenu.

Hatimaye, namshukuru Rachel Maina kwa kunifanyia kazi bora ya kuipiga chapa tasnifu hii. Kwenu nyote, Mungu awabariki.

# IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia mtindo katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.* Tasnifu hii ina sura tano.

Katika sura ya kwanza, tumegusia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia tete,upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti, msingi wa nadharia ya utafiti na njia tulizotumia katika utafiti huu.

Kuhusu sura ya pili, tumechanganua mtindo wa sintaksia katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.* Tumejadili ukiushi wa vipashio katika sentensi, urefu na ufupi wa sentensi na nafasi ya uakifishi katika sintaksia ya diwani yenyewe.

Sura ya tatu imeangazia ukiushi wa kisemantiki katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.* Tumechambua matumizi ya methali, semi, tamathali za usemi na mbinu nyingine za lugha.

Katika sura ya nne, tumeshughulikia matumizi ya msamiati kwa jumla katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.* Tumechunguza namna mwandishi alivyoteua msamiati wake ili kuwasilisha ujumbe wake.

Sura ya tano ina hitimisho la utafiti. Pia, imegusia umuhimu wa utafiti huu na kutoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.*

# YALIYOMO

**Ukurasa.**

UNGAMO ..... i
TABARUKU ..... ii
SHUKRANI ..... iii
IKISIRI ..... iv
YALIYOMO ..... v

**SURA YA KWANZA ..... 1**
1.0 Utangulizi ..... 1
1.1 Tatizo la Utafiti ..... 3
1.2 Madhumuni ya Utafiti ..... 4
1.3 Sababu Za Kuchagua Mada Hii. ..... 4
1.4 Nadharia Tete ..... 5
1.5 Upeo Na Mipaka ya Utafiti ..... 5
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii. ..... 6
1.7 Msingi wa Nadharia ya Utafiti ..... 9
1.8 Njia za Utafiti ..... 12
Tanbihi ..... 13

**SURA YA PILI ..... 14**
**MTINDO WA SINTAKSIA KATIKA *ARUSI YA BULDOZA* ..... 14**
2.0 Utangulizi ..... 14
2.1 Ukiushi Katika Mpangilio wa Vipashio Katika Sentensi ..... 15
2.1.1Ukiushi katika Nomino ..... 15
2.1.2Ukiushi Katika Vitenzi ..... 19
2.1.3Ukiushi Katika Vielezi ..... 19
2.1.4Ukiushi Katika Viunganishi ..... 21
2.1.5Ukiushi Katika Vihusishi ..... 23
2.2 Sentensi Katika *Arusi ya Buldoza*. ..... 24

2.2.1Sentensi Fupi. ....24
2.2.2 Sentensi Ndefu....26
2.3 Nafasi ya Uakifishi Katika Sintaksia....27
2.4 Hitimisho....32
Tanbihi....34

**SURA YA TATU....35**
**UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA *ARUSI YA BULDOZA*....35**
3.0 Utangulizi....35
3.1 Methali....35
3.2 Semi....38
3.3. Tamathali za Usemi....40
3.3.1Tashbihi....40
3.3.2 Sitiari....42
3.3.3 Tashhisi....44
3.3.4 Tasifida....45
3.3.5 Chuku....47
3.3.6 Tabaini....49
3.3.7 Maswali ya Balagha....50
3.3.8 Dhihaka....51
3.4 Mbinu Nyingine za Lugha....52
3.4.1 Majazi....52
3.4.2 Takriri....54
3.4.3 Tanakali za Sauti....55
3.4.4 Mdokezo....56
3.4.5 Kuchanganya Ndimi....57
3.4.6Nidaa....58
3.4.7.Ritifaa....59
3.4.8 Taswira....60
3.5 Hitimisho....61
Tanbihi....62

**SURA YA NNE** .......... **63**

**MATUMIZI YA MSAMIATI KATIKA *ARUSI YA BULDOZA*** .......... **63**

4.0 Utangulizi .......... 63

4.1 Msamiati wa Lahaja ya Kipemba. .......... 63

4.2 Msamiati wa Utohozi. .......... 65

4.3 Msamiati wa Kisitiari Katika Vichwa vya Hadithi. .......... 68

4.4 Ukiushi Katika Maumbo ya Maneno .......... 70

4.5 Ukiushi Katika Ngeli za Maneno .......... 71

4.6 Msamiati wa Sajili .......... 72

4.7 Hitimisho .......... 74

Tanbihi .......... 75

**SURA YA TANO** .......... **76**

**HITIMISHO** .......... **76**

5.0 Utangulizi .......... 76

5.1 Muhtasari wa Matokeo .......... 76

5.2 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi .......... 78

**MAREJELEO** .......... 79

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Mtindo katika fasihi hurejelea matumizi ya lugha.[1] Hii ni dhana muhimu kwa sababu inahusu tofauti iliyopo baina ya fasihi na maandishi ya kawaida. Lugha ya fasihi ni ya kihisia na inabeba kiimbo na mkabala wa mwandishi. Mbali na kuwasilisha ujumbe fulani, lugha ya fasihi inamshawishi msomaji ili kujaribu kuuathiri na pengine kuubadilisha msimamo wake. Ili kumwathiri msomaji kihisia na kimawazo, msanii huifinyanga lugha yake kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kubuni tamathali za semi, wizani na hata ukiushi wa kaida za kisarufi.

Baadhi ya wataalamu na wanadharia wanaona mtindo kuwa ni mchanganyiko wa mambo makubwa mawili. Mambo hayo ni wazo (maudhui) la msanii linaloelezwa na jinsi wazo hili linavyoelezwa na msanii[2]. Nadharia hii inauangalia mtindo kama kitu chenye mchanganyiko uelezeao uhusiano uliopo kati ya mwandishi na kazi anayoifanya. Jinsi jambo linavyosemwa husaidia kuelezea na kufafanua maana ya kile kinachosemwa.

Katika uandishi wa kifasihi, mtindo pia unaweza kuwa ni tabia ya uandishi katika kikundi fulani cha waandishi katika kipindi fulani.[3] Kwa mfano tunaweza kuzungumzia mtindo wa urasimu, urasimu mpya, ramsia na uhalisia au tunaweza kuzungumzia mtindo wa ushairi wa Kiswahili wa karne ya 18 au 19 na mtindo wa ushairi wa kisasa. Hii inatokana na sababu kwamba kikundi fulani cha waandishi chenye kuandika kwa mbinu za aina moja na katika kipindi fulani cha wakati huelekea kufanana kwa kiasi fulani katika

uandishi wao. Inawezekana pia waandishi wanaotoka sehemu moja wakafanana kimtindo. Kwa mfano waandishi wa Mvita (Mombasa) hasa washairi wanatofautiana na waandishi wa Tanzania Kisiwani.

Wakati mwingine, mtindo unaangaliwa kama tabia ya mtu binafsi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha katika kutumia lugha. Mazoea hayo ya mwandishi ya kuandika, kuteua msamiati, tamathali za semi, taswira na uakifishi na mengine yanampambanua mwandishi huyo na wenzake. Waandishi wanatofautiana katika mitindo kwa kuzingatia utofauti wa dhamira, nafsi ya msanii na kipindi alichoandikia hadithi ama kazi yake ya sanaa. Ingawa waandishi wa Kiswahili wanatumia lugha ya Kiswahili, kila mwandishi ana mtindo wake wa kuyaelezea mambo yake.[4]

Mtindo pia unaangaliwa kama ukiushi. Neno ukiushi linatokana na kitenzi 'kiuka'. Kukiuka ni kwenda kinyume au kufanya jambo jinsi lisivyostahili kufanywa. Ukiushi ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea sifa za kimtindo ambazo sio za kawaida na zinaelekea kwenda kinyume na matarajio au sifa za kimatumizi ya lugha zilizopo katika jamii fulani wakati fulani maalum. Mwandishi anaweza kufanya ukiushi unaojitokeza katika viwango kadhaa. Kuna aina nyingi za ukiushi: kisintaksia, kisemantiki, kimsamiati, kisarufi, kifonolojia au wa kihistoria.

Kwa upande wa mwandishi, mtindo unatawaliwa na mambo kadhaa. Kwanza, ni nia na lengo la mwandishi. Pili, ni mtazamo na msimamo wake. Mtazamo wa mwandishi unahusu maono yake juu ya suala zima au masuala anayoyaangalia katika kazi yake.

Mtindo unaweza kutokana na mazingira ya elimu ya mwandishi. Kiwango cha elimu pia kinaweza kuongeza ufanisi wa uandishi wa hadithi fupi. Mwandishi kwa kutumia stadi alizojifunza katika elimu yake, anaweza kuziandika hadithi vizuri. Kwa misingi hiyo, maoni yetu ni kwamba Said A. Mohamed ametumia mtindo katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* kwa namna yake ili kuwasilisha dhamira na maudhui yake kwa njia mwafaka.

Katika sura hii ya kwanza, tumejadili mambo yafuatayo: kwanza, tumefafanua tatizo letu la utafiti na kisha kuyataja madhumuni yetu ya utafiti na sababu zetu za kuchagua mada hii. Aidha, tumetaja nadharia tete ya utafiti wetu na pia kuonyesha upeo na mipaka ya utafiti huu. Mbali na hayo, tumeeleza yale yaliyoandikwa kuhusu somo letu la utafiti. Hatimaye tumefafanua msingi wa nadharia ya utafiti na tumehitimisha kwa kueleza njia tulizotumia katika utafiti wetu.

### 1.1 Tatizo la Utafiti

Baada ya kusoma hadithi fupi katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* kwa makini, tumegundua kuwa Said A. Mohamed ametumia mtindo kwa upekee fulani. Namna alivyofanikiwa kuwasilisha ujumbe wake na kuacha athari kwa wasomaji imetegemea pakubwa namna alivyoteua na kutumia lugha. Kutokana na sababu hiyo, pana haja ya kuchunguza upekee wake wa matumizi ya lugha katika kazi hii.

Diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* tunayoihakiki kimtindo ilichapishwa mnamo mwaka wa 2005. Katika uchunguzi wetu, tumegundua kuwa haijahakikiwa na mtaalam yeyote hasa kuhusu mtindo alioutumia mwandishi. Hivyo basi tumeamua kuhakiki namna msanii huyu ametumia mtindo kuwasilisha dhamira, falsafa na mawazo yake. Kwa kuchanganua mtindo katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*, tutaliziba pengo hilo na kutoa mchango wetu wa kitaaluma.

### 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la kufanya utafiti huu ni kuchunguza mtindo katika hadithi fupi za diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*.

### 1.3 Sababu Za Kuchagua Mada Hii

Kwanza, katika uchunguzi wetu, hatujapata ithibati yoyote ya kuonyesha kuwa kuna utafiti wowote uliokwisha kufanywa kuhusu diwani hii kwa upande wa mtindo. Kwa hivyo, utafiti wetu utaliziba pengo hili.

Tofauti na diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* inayohusisha hadithi za Said A. Mohamed tu, diwani nyingi huhusisha hadithi za waandishi tofauti. Mifano mwafaka ni: *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000), *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *na Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (2006) miongoni mwa zingine nyingi. Kwa hivyo, tunanuia kuchunguza upekee wa msanii huyu kuhusu mtindo wake katika kazi hii.

Mhakiki mzuri hutumia mtindo, kama kigezo cha kutathmini jinsi msanii hupitisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Ikiwa msanii atatumia mtindo barabara, bila shaka ujumbe wake utaifikia hadhira kwa njia nzuri na atakuwa amefanikiwa katika lengo la kazi yake. Kwa sababu ya uzito wa jukumu lake, tumechagua kuhakiki mtindo katika kazi hii ili kuonyesha mchango wake ambao unatokana na uamili wake katika fasihi.

Mtindo katika utanzu wa hadithi fupi haujashughulikiwa sana kama katika tanzu zingine za fasihi andishi ya Kiswahili. Tunaamini basi kwamba utafiti huu utatoa mwanga wa kuhakiki mtindo katika utanzu huu kwa vile watafiti wa baadaye katika utanzu huu watakuwa wanarejelea mchango wa kazi hii kimtindo.

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i) Kuna ukiushi wa mtindo katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.*

ii) Ukiushi wa mtindo unategemea uteuzi wa matumizi ya lugha ya msanii katika diwani ya Arusi *ya Buldoza na Hadithi Nyingine.*

## 1.5 Upeo Na Mipaka ya Utafiti

Said A. Mohamed ameandika diwani tatu za hadithi fupi ambazo ni: *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine ( 2002), Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine ( 2005)* na *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*( 2005). Hatujachunguza mtindo katika diwani hizo zote. Ili

kufanya utafiti wa kina, tumechanganua mtindo katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* tu. Tumechagua kuchunguza mtindo katika diwani hii na kuacha nyingine kwa vile Said A. Mohamed ametumia lugha yenye ukiushi mwingi kisintaksia, kisemantiki na kimsamiati. Isitoshe, ametumia mtindo wa uhalisia mazingaombwe[5] katika hadithi ya 'Arusi ya Buldoza'.

Katika kuchunguza mtindo wa mwandishi katika diwani hii, tumezingatia matumizi ya lugha na athari yake katika kuleta mvuto wa kisanaa. Tumechanganua matumizi ya lugha katika kiwango cha kisintaksia, semantiki na msamiati.

### 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii

Mohamed S. A. (1995) katika kitabu chake *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi,* amezungumzia mtindo kwa kiasi fulani. Amefafanua maana ya mtindo na kuangalia dhana mbalimbali za mtindo kama vile: mtindo kama nyenzo zinazofumbata wazo kuu, mtindo kama mtu mwenyewe, mtindo kama jumla ya tabia za lugha za kikundi au wakati fulani na mtindo kama kuukimbia ukawaida. Mjadala wake kuhusu mtindo umekuwa wa manufaa kwetu kwa sababu tumechunguza mtindo wa Said A. katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.*

Mbatiah M. (2000) ambaye amehariri diwani ya *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* amegusia suala la mtindo katika hadithi fupi. Amefafanua dhana ya mtindo na kuonyesha kuwa mtindo huhusishwa na maudhui. Mchango wake ni muhimu katika kazi yetu kwa vile amejikita katika hadithi fupi.

Msokile M. (1992) amejadili vipengele mbalimbali vya fani katika *Misingi ya Hadithi Fupi.* Moja kati ya vipengele hivyo anavyoshughulikia ni mtindo. Anadokeza mtindo kama mtu mwenyewe na mtindo kama tabia ya uandishi katika kipindi fulani cha mfumo fulani wa maisha ya mtu. Aidha, anaeleza vipengele vya mitindo kuwa ni: uchaguzi na maneno, matumizi ya taswira na ishara, maelezo na masimulizi miongoni mwa mengine. Uchambuzi wake wa mtindo umetuwekea mhimili mzuri wa kuchambua mtindo katika tasnifu yetu.

Kibera V. (1988) amehariri diwani ya hadithi fupi *An Anthology of East African Short Stories.* Katika kazi hii amechunguza masuala katika hadithi fupi kwa njia wazi. Amejadili sifa za hadithi fupi kama vile urefu, wahusika, ploti, mandhari na maudhui. Pia ameshughulikia sifa za muundo wa hadithi fupi. Isitoshe, ameangazia mtindo wa mwandishi katika hadithi fupi. Maoni yake juu ya mtindo wa mwandishi yametuelekeza katika utafiti huu.

Mohochi E. (1995) katika tasnifu yake ya uzamili "Fani Katika Hadithi Fupi za Kiswahili", amechanganua vipengele vinne vya fani ambavyo ni: wahusika, ploti, lugha na usimulizi. Amehakiki hadithi nne za waandishi tofauti ambazo ni 'Wasubiri kifo' ya E. Kezilahabi, 'Siri ya Bwanyenye' ya M. Mulokozi, 'Kicheko cha Ushindi' ya Mohamed S. Mohamed na 'Msiba wa Pamoja' ya S. A. Mohamed. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu inaangazia kipengele cha mtindo ambacho ni lugha.

Mbuthia E. (2005) katika tasnifu yake ya uzamifu "A Stylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories" amehakiki kipengele cha mtindo na maudhui kwa kina. Amechanganua diwani kumi na nne za Kiswahili akianza na zile za awali mpaka zile za kisasa. Uhakiki wake wa mtindo umetufaa katika kuendeleza tasnifu yetu kwa kurejelea baadhi ya vipengele vya mtindo alivyovijadili.

Indangasi H. (1988) katika kitabu chake cha *Stylistics* amezungumzia masuala kadhaa ya elimu-mitindo. Amezungumzia historia ya elimu-mitindo na viwango vya kuchunguza mtindo kama vile fonolojia, sintaksia, msamiati, semantiki na tamathali za usemi. Uchanganuzi huu umetupatia mwelekeo mzuri wa kuchambua kazi yetu kwa vile tumeshughulikia matumizi ya lugha katika kiwango cha sintaksia, semantiki na msamiati.

Leech G. na Short M. (1981) katika *Style in Fiction* wameangalia mawanda ya mtindo. Pia wamejadili kuhusu nadharia ya elimu-mitindo. Isitoshe, wameangazia kuhusu uhusiano wa mtindo na maudhui. Mbali na hayo wameainisha viwango vya kuchanganua mtindo. Viwango hivyo ni: kiwango cha semantiki, sintaksia na kifonolojia. Ingawa kazi yao imejikita katika tanzu zote za fasihi, mchango huu umetuongoza katika kuchanganua mtindo katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*.

Wales K. (2001) katika kamusi yake *A Dictionary of Stylistics,* amefafanua kwa kina kuhusu dhana za mtindo na elimu-mitindo. Aidha, ametoa fafanuzi mwafaka za tamathali anuwai za usemi. Hivyo basi, kamusi hii imetufaa katika kurejelea dhana mbalimbali katika utafiti wetu wa mtindo.

Kitsao J. (1975) amehakiki mtindo katika kazi za kinathari za Kiswahili katika tasnifu yake ya "A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts". Katika tasnifu yake, amefafanua dhana ya elimu-mitindo na mtindo. Ameonyesha namna mtindo hujitokeza katika kazi ya kifasihi. Baada ya kufanya hivyo amechunguza namna mtindo umejitokeza katika kazi mbalimbali za kifasihi alizozishughulikia. Uhakiki huu umetufaa pia kwa kutupatia mwelekeo wa kazi hii.

Mwanzi H. (1995) naye amehakiki kipengele cha mtindo katika tasnifu yake ya uzamifu "The Style of the Short Story in Kenya: An Analysis of the Short Stories of Ngugi wa Thiong'o, Leonard Kibera and Grace Ogot". Utafiti wake umejikita katika mitindo ya waandishi hawa katika kazi zao. Uchanganuzi wake ni muhimu kwa vile umetupatia mwanga wa kuhakiki mtindo wa msanii katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*.

**1.7 Msingi wa Nadharia ya Utafiti**

Nadharia tunayoitumia kuangazia mtindo katika utafiti wetu ni ya elimu-mitindo. Leech G. na Short M. (1981: 13) wanafasili elimu-mitindo kuwa ni uchunguzi wa mtindo. Aidha, wanafasili mtindo kuwa ni namna lugha inavyotumiwa katika muktadha na mtu fulani kwa lengo fulani. Wanasisitiza kuwa katika upana wake, neno mtindo linatumika kwa usemi wa kimdomo na maandishi katika masuala ya kifasihi na yasiyo ya kifasihi lakini mara nyingi mtindo huhusishwa na matini.

Kwa mujibu wa Wamitila K. (2003: 39) elimu-mitindo ni dhana inayotumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi na uchanganuzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi za kifasihi. Ni taaluma iliyoko kati ya uchunguzi wa lugha na uchunguzi wa fasihi au jinsi lugha inavyotumika katika matini au kazi za kifasihi. Huweza kuhusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi fulani na zinazomtambulisha mwandishi anayehusika.

Lengo hasa la elimu-mitindo ni kueleza uhusiano uliopo baina ya lugha na jukumu la kisanaa. Kutokana na mkabala wa kiisimu, swali linalojitokeza ni je, 'kwa nini mwandishi amechagua kujieleza kwa namna alivyofanya?' Kwa upande mwingine, kwa mkabala wa mhakiki swali linakuwa, 'Ni kwa namna gani ujumi umepatikana kwa kutumia lugha?'[6]

Wales, K. (2001:372) anasema kwamba namna mtindo unavyoweza kuchunguzwa kwa njia mbalimbali ndivyo elimu-mtindo inavyoweza kuangaliwa kwa mikabala tofauti. Tofauti za elimu-mitindo inatokana na athari za matawi tofauti ya kiisimu na uhakiki wa kifasihi.

Uchunguzi wa nadharia ya elimu-mitindo katika karne ya 20 ulibadilisha na kupanua uchunguzi wa awali wa ufasaha katika usemaji. Kufuatia kuchapishwa kwa majuzuu mawili ya tasnifu kuhusu elimu-mitindo ya Kifaransa na Bally (1909) ambaye alikuwa mwanafunzi wa mwana-miundo de Saussure, shauku katika elimu-mitindo ilianza kuenea polepole katika bara la Ulaya kupitia kazi ya Spitzer (1928, 1948) na wengine. Katika

miaka ya 1960 ndipo uchunguzi wa elimu-mitindo ulistawi nchini Uingereza na Marekani, kutokana na msukumo wa maendeleo baada ya vita vya pili vya dunia katika isimu elekezi hasa katika sarufi.

Kwa namna nyingi, elimu-mitindo inakaribiana sana na uhakiki wa kifasihi na uhakiki wa kiutendaji. Mara nyingi kazi inayochunguzwa ni ya kifasihi; na msisitizo huwekwa kwenye matini. Lengo la uchunguzi mwingi wa kimtindo sio tu kueleza sifa za matini tu, bali ni kuonyesha uamilifu na umuhimu wake katika kufasiri matini.

Nadharia ya elimu-mitindo haina upendeleo kwa maana kwamba ina utaratibu, ujarabati, uchanganuzi, mwambatano na maridhiano. Kwa sababu hiyo, elimu-mitindo inaendelea kujitokeza na istilahi mpya kutokana na maendeleo mapya katika isimu. Katika mwisho wa miaka ya 1960, sarufi zalishi ilistawi ilhali katika miaka ya 1970 na 1980, uchanganuzi wa kidiskosi na amali ulistawi. Katika miaka ya 1990 uhakiki na uchanganuzi wa kidiskosi ulishamiri.

Nadharia ya elimu-mitindo wakati mwingine hukanganya kwa kuitwa kuwa ni elimu-mitindo ya kifasihi au elimu-mitindo ya kiisimu. Inaitwa elimu-mitindo ya kifasihi kwa sababu inaelekea kuangazia matini za kifasihi. Kwa upande mwingine inaitwa elimu-mitindo ya kiisimu kwa sababu zana zake muhimu huchotwa kutoka kwa isimu. Hata hivyo, elimu-mitindo ya kiisimu inatumiwa kurejelea aina ya mtindo ambao lengo lake sio tu matini za kifasihi, lakini ni kutengeneza upya kielelezo kizuri cha kiisimu ambacho kinaweza kutumika kwa uchunguzi zaidi kiisimu au kimtindo.

Elimu-mitindo inaweza kutumika kama dhana ya kijumla ambayo inahusu uchanganuzi wa lugha anuwai zisizo za kifasihi au sajili. Kwa sababu ya upeo huo mpana, elimu-mitindo inakaribiana sana na kazi zinazofanywa katika isimujamii. Kwa mfano, isimujamii huchunguza lugha ya waandishi inavyochukuliwa kama makundi ya kijamii.

Indangasi H. (1988: 10) anaelezea kwa uwazi uamili wa elimu-mitindo. Anasema kwamba elimu-mitindo imesaidia kuondoa maoni ya wahakiki yasiyo na msingi kuhusu kazi za kifasihi na hasa kuhusu lugha za kazi hizo. Vile vile, elimu-mitindo imesaidia kuondoa utata uliokuwapo kati ya fani na maudhui kwa kutoa maelezo ya lugha ya kifasihi kama kitu kinachoweza kutabirika. Isitoshe, elimu-mitindo hutupatia mbinu za kuchanganua upekee wa kazi za kifasihi, ama zilizoandikwa au simulizi.

## 1.8 Njia za Utafiti

Kuna mbinu nyingi za utafiti kutegemea aina na malengo ya utafiti. Katika utafiti huu, tumetumia mbinu zifuatazo ili kufanikisha utafiti wetu. Kwanza, tumesoma na kuchanganua hadithi zote katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* huku tukichunguza namna vipengele vya mtindo vimejitokeza humo. Pili, tumerejelea makala, tasnifu na vitabu vya kitaaluma ambavyo vimeshughulikia mtindo ili kupata uelewa zaidi wa mada hii.

Hali kadhalika, tumekuwa na mazungumzo ya ana kwa ana na walimu mbalimbali hasa wa fasihi na kupata maoni na ushauri wao ili kuboresha utafiti huu. Kwa jumla, utafiti mwingi umefanyiwa maktabani.

**Tanbihi**

1 Mbatiah M. *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*, Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation, 2000, uk. xv.

2 Msokile M. *Misingi ya Hadithi Fupi*, Dar es Salaam, Dar es Salaam Univeristy Press, 1992, uk. 66.

3 Mohamed S. A. *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi,* Nairobi, E.A.E.P, 1995, uk. 44.

4 Kama namba 2, uk. 66.

5 Dhana hii inahusu mtindo hasa wa sanaa unaochanganya uhalisia (ukweli wenye mantiki) na mazingaombe (uchawi).

6 Leech G. na Short M. *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose,* London, Longman Group Limited, 1981, uk. 13.

# SURA YA PILI

## MTINDO WA SINTAKSIA KATIKA *ARUSI YA BULDOZA*

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunachunguza kitengo cha lugha ambacho kinashughulikia matumizi ya sentensi katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.* Kitengo hiki kinaitwa sintaksia. Habwe J. na Karanja P. (2003:125) wanafasili sintaksia kuwa ni utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa sentensi na elementi nyingine zinazounda sentensi kama vile kategoria za maneno[1], virai[2] na vishazi[3]. Muundo wa sentensi hurejelea jinsi vipashio vyake huungana na kuhusiana ili kuunda sentensi yenye maana. Sentensi ni kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo chenye kuleta maana kamili.

Lengo letu ni kuchunguza namna mwandishi amekiuka matumizi ya kawaida ya mpangilio wa maneno katika sentensi ili kuwasilisha ujumbe wake. Katika kufanya hivyo tunatoa mifano anuwai ya ukiushi, athari za ukiushi na ufanifu wa ukiushi mbali na kuonyesha namna sentensi hizo zingeandikwa katika hali ya kawaida. Ukiushi ni mbinu mojawapo ya mtindo wa mwandishi katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.*

Aidha, tunaangazia nafasi ya uakifishi wa mwandishi katika sintaksia. Tunaangalia ni alama gani za uakifishi ambazo amezitumia sana, ni kwa nini anazitumia na namna zinavyoathiri sintaksia katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.*

Kila lugha ina utaratibu wake maalum na mpangilio wa maneno katika sentensi. Utaratibu huo usipofuatwa, kitakachotokea ni tungo au sentensi zisizokubalika. Lugha ya Kiswahili ina kanuni kwamba sentensi lazima iwe na kiima na kiarifu. Kiima ni sehemu ya kirai nomino ambayo inatolewa habari zaidi. Kwa upande mwingine, kiarifu ni taarifa inayotolewa juu ya kiima.

## 2.1 Ukiushi Katika Mpangilio wa Vipashio Katika Sentensi

Massamba D. na wenzake (1999:34) wanasema kwamba sarufi miundo ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Vipashio hivyo ni kama nomino, vivumishi, viunganishi, vielezi na vihusishi. Tunachunguza jinsi vipashio hivi vimepangwa kwa mtindo usio wa kawaida na namna vinavyoathiri sintaksia katika diwani yenyewe.

### 2.1.1 Ukiushi Katika Nomino

Nomino ni neno linalotaja jina la mahali, mtu, kitu, hali au tendo. Katika lugha ya Kiswahili, aghalabu nomino huja mwanzo, kivumishi hufuata kama kipo, kisha kitenzi na baadaye kielezi kama kipo. Katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine,* Mwandishi amekiuka mpangilio huo wa kuanza na nomino katika baadhi ya sentensi.

Katika hadithi 'Mtego' tunasoma kuwa ' Kijasho chembamba Salamuu kilimtiririka' (uk. 53). Ingawa mwandishi ameanza kwa nomino 'jasho', ameweka nomino 'Salamuu' mahali si pake. Huo ni ukiushi. Sababu ya kufanya hivyo ni kusisitiza na kutufanya

tuelewe hali iliyomkumba mhusika Salamuu. Mwandishi amefanikiwa kusawiri hali inayomkumba Salamuu baada ya kupokea barua kutoka kwa Mchawi (Kassim) mbali na kuongeza ujumi wa kisanii. Kikawaida, sentensi hiyo ingekuwa:

'Kijasho chembamba kilimtiririka Salamuu'.

Katika hadithi 'Mhogo', mheshimiwa anatoa hotuba kwa wananchi kwa kuwahimiza wale mhogo kwa wingi badala ya kula wali na ngano. Tunasoma:

Mhogo wananchi ndicho chakula chetu. (uk. 66)

Katika dondoo hili, mheshimiwa anasisitiza ujumbe wake kwa kutanguliza nomino 'mhogo'. Katika usemi wa kawaida tungetarajia mheshimiwa kuitamka sentensi hiyo ifuatavyo:

'Wananchi, mhogo ndicho chakula chetu'

Aidha, kuna mbinu ya takriri katika sentensi hiyo. Takriri ni mbinu ya kifasihi ya kurudia neno, mstari au vifungu fulani kwa ajili ya kusisitiza. Kuna takriri neno, konsonanti-irabu na takriri konsonanti. Kwa hivyo, kuna takriri ya konsonanti 'ch' katika sentensi hiyo. Imetumika ili kuleta wizani ya namna fulani katika sentensi.

Kwingineko katika hadithi 'Uhuru wa Subira' tunapata mfano mwingine wa ukiushi wa nomino. Mrisho, mume wa Subira anaporudi nyumbani saa kumi alfajiri anamwambia Subira afungue mlango akiwa na mpango wa kumpiga. Hata hivyo, Subira hafungui mlango. Mrisho anapopiga mlango teke na kuingia ndani, anashtuka kupata maiti ya Subira ikining'inia juu ya boriti ya dari. Tunasoma:

> Alikuwa kesha geuka kutaka kutoka nje, ndipo alipotupa jicho juu na pale darini...Alipata mshtuko Mrisho. Maiti ya Subira ilikuwa ikining'inia kwenye boriti ya dari.
> (uk. 97)

Katika dondoo hili, mwandishi ametanguliza nomino 'mshtuko' kwa sababu ya kusisitiza hali iliyomkabili Mrisho. Mbali na msisitizo huo, takriri ya konsonanti 'sh' inajitokeza katika neno 'mshtuko' na 'Mrisho'. Mapigo hayo yanaleta athari ya wizani katika sentensi hii. Katika hali ya kawaida sentensi hiyo ingekuwa:

'Mrisho alipata mshtuko.'

Sentensi hii ya kawaida haingeleta uzito wa mshtuko alioupata Mrisho kama sentensi iliyotangulia.

Katika 'Maskini Haokoti' tunapata namna msichana kwa jina Halima aliingia chumbani mwa Mussa. Tunasoma kuwa:

> Buibui lake kaliacha sesa ili kutoa nafasi kwa Mussa kuona kifua kikuza kilichoumuka – dodo huku, na dodo huku; katikati msingi ambapo matone ya jasho Halima yalimtiririka.
> (uk. 148)

Badala ya kuanza na kitenzi 'yalimtiririka' baada ya 'matone ya jasho', mwandishi anaanza kwa nomino 'Halima' kisha kitenzi 'yalimtiririka'. Kikawaida sentensi hiyo ingekuwa:

'...katikati ya msingi ambapo matone ya jasho yalimtiririka Halima.'

Katika 'Pigo la Tamaa' Said anapoenda kwao Salma Masoud kumweleza kuwa wazazi wake wamekubali amuoe Salma hata kama ni kiwete, anapata mazishi yakiandaliwa. Mussa, kakake Salma anamwambia kuwa Salma alijiua kwa kumkosa Said. Ndiposa tunasoma kuwa:

Said moyo ulimpasuka. Damu ilichemka (uk. 167)

Kwa kutaja jina 'Said' mwanzoni mwa sentensi, mwandishi anaonyesha uchungu aliopata Said kwa kuambiwa kuwa mpenzi wake amejiua. Tunapata hisia ya huzuni na simanzi moyoni mwa Said. Katika hali ya kawaida ya kutosisitiza ingekuwa:

'Moyo ulimpasuka Said.'

### 2.1.2 Ukiushi Katika Vitenzi

Kitenzi ni neno ambalo huarifu kitendo kinachofanyika. Katika lugha ya Kiswahili aghalabu kitenzi huja baada ya kiima ambacho hubeba nomino. Katika diwani hii, mwandishi ameanza sentensi kwa kitenzi katika baadhi ya hadithi zake. Kwa mfano katika 'Arusi ya Buldoza' tunasoma:

Pu! Ulimng'oka moyo Mjaka. (uk. 7)

Mwandishi ametumia kielezi 'pu!' kuonyesha jinsi moyo wa Mjaka ulivyodunda baada ya kusikia sauti ya kwenzi za farasi alipokuwa juu ya kijilima akipumzika. Kielezi 'pu!' pia ni tanakali ya sauti inayoiga namna moyo ulivyompiga. Baadaye, msanii anaanza sentensi kwa kitenzi 'ulimng'oka' kwa sababu anatilia mkazo kitendo cha moyo kumng'oka Mjaka.

### 2.1.3 Ukiushi Katika Vielezi

Kielezi ni kipashio katika sentensi ambacho hutumika kuelezea jinsi, wakati na mahali kitendo kinafanyika. Kwa hivyo, kuna vielezi vya jinsi au namna, vielezi vya wakati na vya kuonyesha mahali. Kuna mifano kadhaa ya ukiushi katika vielezi katika hadithi tofauti tofauti. Kwa mfano, katika 'Arusi ya Buldoza' tunapata mhusika Mjaka akiwa juu ya kijilima ambapo anapumzika baada ya shughuli ngumu ya kujenga nyumba ya mawe ili amuoe Kilua. Akiwa juu ya kijilima, anaanza kufikiria juu ya nchi na jamii yake. Wapi inatoka, wapi ipo na wapi inaelekea. Tunaelezwa:

Kila siku, alilaani visirani vilivyoiandama nchi yake. (uk. 6)

'Kila siku' ni kielezi cha wakati. Kielezi hiki kinafanya kazi ya kusisitiza ni mara ngapi Mjaka alifanya kitendo cha kulaani. Sentensi hiyo ingekuwa:

'Alilaani kila siku, visirani vilivyoiandama nchi yake.'

Aidha, katika hadithi hii, tunaelezwa namna Mjaka alivyoteremka kutoka juu ya kijilima aliposikia sauti na kwenzi za farasi kutoka nyumbani kwake. Tunasoma:

Mbio, mbio, mbio, akakiteremka kile kijilima. (uk. 7)

'Mbio' ni kielezi cha jinsi Mjaka alivyoteremka kutoka juu ya Kijilima alipokuwa amepumzika. Mbali na kuwa kielezi, neno 'mbio' limetumika kama mbinu ya takriri ya kusisitiza kitendo cha kuteremka. Ni aina ya takriri neno. Athari ya matumizi ya neno 'mbio' ni kwamba inaleta sifa ya utambaji wa hadithi katika fasihi simulizi. Urudiaji huo unamchorea msomaji picha na pia kumburudisha anapoisoma hadithi.

Katika hadithi 'Dhuluma Inamojificha' tunaona namna Jabu, mume wa Siti alivyojitahidi kumwibia mama mmoja mkoba wake kusudi apate pesa za kumnunulia mkewe mavazi ya arusi. Tunasoma kuwa:

Nyatu, Nyatu...alinyatia nyuma ya huyo mwanamama. (uk. 15)

'Nyatu, nyatu' ni kielezi cha jinsi Jabu alivyomnyemelea mwanamke huyo kwa kusudi la kunyakua mkoba wake. Aidha, ni takriri neno linalosisitiza kitendo cha kumnyemelea kutoka nyuma. Kikawaida sentensi hiyo ingekuwa:

'Alinyatia nyatu nyatu nyuma ya huyo mwanamama.'

Katika hadithi 'Uhuru wa Subira' tunapata namna Mrisho alivyomtafuta mkewe Subira chumbani alipotoka kulewa. Tunasoma kuwa:

Jicho <u>chini</u> aliangaza chumba chote. (uk. 97)

'Chini' ni kielezi cha mahali ambapo Mrisho alimtafuta mkewe Subira. Kimewekwa kabla ya kitenzi 'aliangaza' kwa msisitizo wa mahali. Vile vile kuna takriri ya konsonanti 'ch' katika sentensi hiyo ambayo inaleta mapigo fulani. Ikiwa sentensi hiyo ingeandikwa kikawaida ingekuwa:

'Aliangaza jicho chini chumba chote.'

### 2.1.4 Ukiushi Katika Viunganishi

Viunganishi ni maneno yanayounganisha neno na neno, vikundi vya maneno au sentensi. Baadhi ya viunganishi ni kama 'na', 'wala', 'au' ' tena' na ' lakini'.

Mwandishi amekiuka matumizi ya viunganishi katika sentensi hasa pale ambapo anaanza sentensi kwa viunganishi. Ametumia sana viunganishi 'na', 'lakini' na ' tena' kama mtindo wake. Kwa mfano katika hadithi 'Dhuluma Inamojificha' tunasoma:

> Siti na khanga yake ya kifua, guu huku, guu kule. Na mkono wake wa kushoto kashikilia shungi la nywele zilizoroa mafuta ya nazi chapachapa.
> (uk. 12)

Mtunzi anaanza sentensi kwa kiunganishi 'na' ambacho kinastahili kuunganisha neno, kifungu cha maneno au sentensi na sentensi. Sababu ya kutumia kiunganishi hicho hapo ni kusisitiza namna alivyoshikilia shungi la nywele mkononi.

Katika hadithi 'Ukarimu wa Mwihaji' tunampata Mwihaji akiwa mahakamani akijitetea dhidi ya kesi inayomkabili ambapo alimuua mheshimiwa aliyefanya mapenzi na mke wake. Tunaelezwa kuwa:

> Nguvu zake zikawa ndiyo badala ya wakili ambaye angemtetea. Tena alimtupia jicho mkewe akamuona hajabadilika, yuko vilevile.
> (uk. 21)

Mwandishi ameanza sentensi kwa kiunganishi 'tena' kwa sababu anatoa nyongeza ya kauli aliyoitoa katika sentensi iliyotangulia.

Kuhusu matumizi ya 'lakini' mwanzoni mwa sentensi, tunasoma katika hadithi 'Riziki Tundu Nyingi' hivi:

> Lakini kwa akina Sururu ambao wameshonana na shida na maafa yaliyozalikana, walitamani gharika ije iteketeze kila kitu cha jiji hili ili kila mtu aanze tena upya na mwanzo.
> (uk. 32)

Msanii ametumia kiunganishi 'lakini' mwanzoni mwa sentensi kwa sababu analinganisha maisha ya akina Sururu ambao ni watu maskini na matajiri wanaoishi katika majumba mazuri na kutembelea magari ya kifahari. Ulinganishi huo unaonyesha uhalisia wa maisha katika miji.

### 2.1.5 Ukiushi Katika Vihusishi

Kihusishi ni neno linaloonyesha uhusiano baina ya neno moja na jingine au maneno mengine katika tungo au kitu kimoja na kingine. Mifano ya vihusishi ni kama 'juu ya', 'kando ya' , 'ndani ya' na 'chini ya'.

Mfano mwafaka wa matumizi ya kihusishi mwanzoni mwa sentensi ni huu katika 'Arusi ya Buldoza' ambapo tunasoma:

> Juu ya kilele cha kilima ndipo ukomo unapomfikisha anapokuwa na mshawasha na wasiwasi ndani ya moyo wake.
> (uk. 4).

'Juu ya' ni kihusihi ambacho kimetumiwa mwanzoni mwa sentensi. Katika kanuni za sarufi ya Kiswahili, kihusishi hakitumiki mwanzoni mwa sentensi. Katika dondoo hili, mwandishi amekitumia ili kutoa msisitizo wa mahali alipo Mjaka.

## 2.2 Sentensi Katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*

Said Ahmed Mohamed amechanganya sentensi fupi na ndefu katika hadithi zake kama mtindo wake wa kujieleza.

### 2.2.1 Sentensi Fupi

Sentensi inaweza kuwa fupi ikiwa na maneno machache mradi tu mwandishi ameeleza wazo lake kikamilifu. Inaweza kuwa ya neno moja, maneno mawili au matatu mradi tu ina kiima na kiarifu ndani yake. Mohamed S. A. (1995: 141) anasema kuwa "kazi muhimu ya sentensi fupi mara nyingi ni kujenga hisia ya uchangamfu, harakati, woga, hofu au wasiwasi." Kwa ajili ya ufupi wa sentensi kunapatikana mapigo ya mizani mafupi mafupi. Mapigo hayo ya mizani yanafanya mtitimo unaokwenda haraka haraka. Mtitimo huo ndio unaosaidia kubainisha hisia mbalimbali.

Katika 'Arusi ya Buldoza' tunaelezwa hali ya furaha ya wanawake wanaocheza nyumbani kwa Mjaka mkesha wa siku ya arusi yake hivi:

> Wamevaa furaha wanawake – nguo ya wakati huu!
> Wanacharaza. Wanakatika. Wananenguka.
> (uk. 1)

Dondoo hili lenye sentensi fupi fupi linaonyesha hisia za furaha na uchangamfu walio nao wanawake hao.

Kwingineko katika hadithi hii, tunampata Mjaka akikimbia kwenda kwake kutoka juu ya kijilima aliposikia ghasia nyumbani kwake. Tunasoma kuwa:

> Alihisi kunatokea kitu kule kwake. Alipiga ukwenzi. Akatimka. (uk. 7)

Sentensi hizi fupi fupi zinatudhihirishia hisia za hofu ya Mjaka. Anapofika kwake, anakuta askari wakipiga watu ovyo. Licha ya hayo anapata kuwa nyumba za watu wengi zimebomolewa na buldoza pamoja na ile yake aliyoijenga kwa taabu kubwa.

Aidha, katika hadithi 'Dakika ya Mwisho', pana matumizi ya sentensi fupi. Msanii ameeleza hali ya Malaika kutomwelewa Yunus wakiwa katika kijikahawa cha *Lover's Corner* kwa setensi fupi fupi. Tunaambiwa:

> Malaika aliemewa. Alitumbua macho. (uk. 59)

Katika 'Mkono wa Salama' mtunzi pia anaonyesha hofu ya Salama juu ya mume wake Simba alipopiga kelele usiku baada ya kushambuliwa na chatu mtoni. Tunasoma:

> Na isitoshe sauti ile ya mumewe ilikuwa na maana moja tu.
> Amesibiwa na jambo! Silaha kibindoni. Ndipo Salama
> alipochukua mundu wake uliokuwa umesimama upenuni.
> Akatoka.
> (uk. 105)

### 2.2.2 Sentensi Ndefu

Hakuna idadi kamili ya maneno iliyotengewa kuhusu sentensi ndefu. Hata hivyo unaposoma kazi fulani, wakati mwingine unakumbana na sentensi ambazo zimetumia maneno kama zaidi ya arobaini tofauti na sentensi fupi ambayo inaweza kuwa ya neno moja. Urefu wa sentensi unatokana na matumizi ya viunganishi kama 'na', 'wala', 'lakini', 'au' na 'tena' ambavyo huunganisha maneno na sentensi kadhaa. Sentensi za aina hiyo huitwa ambatani[4].

Kama anavyosema Mohamed S. A. (1995: 142) sentensi ndefu zenye kufululiza hupunguza mwendo na kwa hivyo badala ya kuwa na mtitimo wa haraka haraka kuna hali ya kudorora. Athari ya matumizi ya sentensi ndefu katika kazi ya kifasihi ni kwamba kunakuwa na hali ya huzuni, msiba, uvivu wa jambo au kutabiri jambo baya linaloweza kutokea. Pia huweza kutumika kama mbinu ya usimulizi au mahubiri.

Matumizi ya sentensi ndefu yanajitokeza katika hadithi 'Ukarimu wa Mwihaji'. Mwandishi anatusimulia sura ya mahakama miaka ishirini iliyopita ikilinganishwa na inavyoonekana kwa sasa. Tunaambiwa:

> Wakati ule kumbi hili, <u>na</u> mahakama nzima, ilikuwa iking'ara weupe wa chokaa iliyoumiza macho, <u>na</u> madirisha <u>na</u> milango iliyosingwa mafuta <u>na</u> vanishi <u>na</u> kuyafanya daima yawe maarusi wasiokonga <u>na</u> zaidi hasa kwa yale matovu <u>na</u> bawabu zao za shaba zilizochukuliwa <u>na</u> kusuguliwa kila saa <u>na</u> vioo vilivyopanguswa kila dakika.
> (uk. 21)

Matumizi ya sentensi ndefu yanajitokeza pia katika hadithi 'Mhogo' kuhusu mheshimiwa mmoja aliyeitisha mkutano wa kuwahutubia wananchi juu ya kula mhogo badala ya wali na ngano. Tunasoma:

> Waliokuja mwanzo ndio waliokaa lakini kaumu ya watu kwa wingi kama huo, walikuwa wamesimama pembeni na wengine wamepanda juu ya miti na wengine wamekaa juu ya vipaa na madomo ya magari. Kila mmoja alikuwa na hamu ya kumsikia kiongozi mashuhuri na kujua kipi muhimu kitachosemwa katika mkutano huo mkubwa ambao umetangaziwa mwezi mzima kwenye redio, televisheni, magazeti na hata kwa upatu.
> (uk. 63)

Kwingineko katika hadithi hii pia tunaambiwa:

> Baada ya hotuba hiyo fupi iliyochukuwa kama dakika tano, lakini iliyogharimu mengi kwa wananchi, mheshimiwa alipeana mikono ya pongezi na waheshimiwa wengine na kisha alipanda gari yake akiandamana na mkururo wake wa polisi, majeshi na wakubwa wengine.
> (uk. 66)

## 2.3 Nafasi ya Uakifishi Katika Sintaksia

Uakifishi ni dhana inayorejelea matumizi mwafaka ya alama mbalimbali katika sarufi ya lugha husika. Uakifishi ni muhimu pia katika kazi ya kifasihi kwa sababu unaathiri namna ujumbe unavyomfikia msomaji.

Katika diwani ya *Arusi ya Buldoza,* mwandishi ametumia baadhi ya alama za uakifishi katika sentensi na hivyo basi kuathiri sentensi kwa namna fulani. Kwa mfano, msanii ametumia nukta tatu yaani (...) mahali kwingi katika hadithi zake. Alama hizi huitwa 'alama za duku duku'. Alama hizi hutumika kudokeza au kuonyesha usemi uliokatizwa katika sentensi. Msemaji kisha huanza sentensi kisha lakini haikamilishi. Wakati mwingine, alama za duku duku huonyesha hali ya kukata kauli ya mtu kabla hajamaliza kuzungumza. Aghalabu, sababu kuu ya kutumia nukta za duku duku ni kuonyesha kusita kwa mzungumzaji.

Kwa mfano, katika hadithi 'Mtego', mhusika Kassim anasita kuzungumza anapopokea barua kutoka kwa Fatma. Barua hiyo iliandikwa na Salamuu. Tunasoma:

> Ule mkono wake uliozoea kuzipokea barua kama hizo
> akazipuuza leo ulitetemeka. "Ngo...ngoja kwanza,"
> alimsimamisha Fatma...
> (uk. 52)

Aidha katika hadithi 'Tofauti' Salim anapoomba msamaha kwa Fadhila kwa kukawia kufika ufuoni, Fadhila anababaika anapomjibu. Tunasoma:

> "Sahamani." Alinguruma Salim.
> "A...at...ata!... 'apana neno,"
> alibabaika Fadhila.
> (uk. 82)

Tunaona kwamba, matumizi ya nukta za duku duku yanaathiri mtiririko mzuri wa sentensi na ujumbe pia. Isitoshe, zinaonyesha mazungumzo ya wahusika katika hali halisi.

Alama ya kuuliza (?) pia imetumiwa sana na mwandishi. Alama hii inapotumika sana, humshirikisha msomaji kwa kumfanya afikirie juu ya hali ya mhusika fulani. Inatumika kuunda sentensi za maswali yasiyohitaji majibu mbali na kujenga taharuki ya aina fulani. Kwa mfano, katika hadithi 'Dhuluma Inamojificha' tunapata swali la balagha kutoka kwa Zaina hivi:

> Kwa kauli hiyo ya Siti, Zaina aliona aubane kimya. Lo, hivi ndivyo dunia hii ilivyobadilika?
> (uk. 12)

Katika hadithi 'Riziki Tundu Nyingi', tunampata Sururu, mhusika mkuu akiwaza juu ya sababu iliyofanya watu wawapatie pesa vipofu wawili walioimba nyimbo kando ya barabara. Tunaambiwa:

> Hakujua kitu gani kilichowafanya watu watoe pesa kuwapa. Ni zile nyimbo za kwaya zinazosikitisha na kuogofya wakati mmoja? ... Ni ule upofu wao? Ni lile gitaa au cherewa? Au ni yale maneno ya wimbo?
> (uk. 36)

Msomaji anaposoma dondoo hili, analazimika kufikiria maswali hayo ya balagha akijaribu kupata majibu yake. Alama ya kuuliza huathiri sintaksia ya kazi husika kwa kufanya sentensi ziwe za maswali wala si sentensi za kutoa taarifa fulani.

Koma (,) ni alama nyingine ya uakifishi iliyotumiwa na msanii kwa namna yake. Kwa kawaida koma hutumika kutoa nafasi ya kupumua katika sentensi msomaji anaposoma na kuorodhesha vitu. Katika diwani hii, mtunzi ametumia 'koma' kutenganisha sentensi ndefu zenye mofimu 'ka' inayoonyesha vitendo vinavyofuatana. Aidha, imetumiwa ili kuepuka kurudia kiima kilichotajwa mwanzoni mwa sentensi.

Kwa mfano, katika hadithi 'Ukarimu wa Mwihaji' tunaelezwa namna Mwihaji alivyomkaribisha mheshimiwa nyumbani kwake kwa mfululizo wa vitendo. Tunasoma:

> Basi Mwihaji a<u>ka</u>mchukua mheshimiwa kwake, a<u>ka</u>mwita mkewe atoe mkeka wao mpya, a<u>ka</u>mtandikia na kisha haraka a<u>ka</u>panda mnazi a<u>ka</u>mwangushia madafu ya kitamli mawili, a<u>ka</u>mchongea.
> (uk. 123)

Mwandishi ametumia 'koma' pamoja na mofimu 'ka' ya kuonyesha vitendo vinavyofuatana ili kusisitiza ukarimu wa Mwihaji kwa mheshimiwa. Mofimu 'ka' inafanya sentensi kuwa changamano. Aidha, hataki kurudiarudia kiima 'Mwihaji". Angerudia kiima kwa kila sentensi, kungetokea hali ya ukinaifu. Ndio maana anatumia 'koma'.

Katika hadithi 'Mtego' tunapata mhusika Salamuu akiwa katika hali mbalimbali. Kwanza, Salamuu alipomsimamisha 'Mchawi' (Kassim) na akapuuza kusimama, Salamuu aliona kuwa ni dharau kubwa. Tunasoma:

> Basi tokea siku hiyo alipotelewa na furaha, akakosa utulivu. Akaghadhibika, akahamanika, akataka amsahau mchawi, lakini wapi mchawi hasauliki.
> (uk. 50)

Baadaye katika hadithi hii, Salamuu aliamua kumwandikia Kassim barua ya kumwonya asimfuatefuate. Tunaambiwa:

> Salamuu hakutaka kufikiri mengi. Alitoka akenda msalani, akakoga, akatawadha, akasali, akanywa kikombe cha kahawa.
> (uk. 51)

Msanii ametumia kistari (-) kwingi katikati ya sentensi hasa pale ambapo anafafanua kitendo, hali, sababu ya kitendo fulani kufanyika au kusisitiza jambo fulani. Kwa mfano, katika hadithi ya 'Arusi ya Buldoza', tunapata wanawake wakicheza densi nyumbani kwa Mjaka. Tunaelezwa:

> Wanawake wanatupa viuno vyao visivyo mifupa chini, baada ya kuvirusha juu kutoa moshi na mvuke na kisha kuvibwaga ardhini, na baadaye hao – kwa uchawi – huvizoazoa na kuvibandika na kuanza kuvisuka tena.
> (uk. 1)

Katika 'Dhuluma Inamojificha' mtunzi anatoa kauli kuwa "Leo ndio leo-kama alivyosema Siti-asiye mwana aeleke jiwe." (uk. 13). Dondoo hili linaonyesha hali ya mhusika Siti kutaka kufanya kitendo chochote ikiwa mumewe hakumnunulia mavazi ya arusi.

Katika hadithi 'Mtego', mwandishi ametumia kistari kutuonyesha sababu ya Kassim kutosimama njiani aliposimamishwa na Salamuu. Tunasoma:

> Alipomaliza tu mechi ya mpira siku ile, alipata taarifa kuwa bimkubwa mzazi wake alikuwa taabani, naye amelazwa hospitali – ikambidi amkimbilie.
> (uk. 51)

Katika kuonyesha namna kistari kinatumika kusisitiza, tunapata mfano huu katika hadithi 'Dakika ya Mwisho':

> Siku nyingine – pahala palepale – saa zilezile – kiti kilekile – meza ileile na kipembe kilekile...
> (uk. 55)

## 2.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeanza kwa kutoa fasili ya istilahi 'sintaksia' ambapo tumesema kuwa ni utanzu wa sarufi ambao unashughulikia muundo wa sentensi na elementi nyingine zinazounda sentensi. Aidha, tumefafanua maana ya setensi kwa kusema kuwa ni tungo inayojitosheleza ambayo huhusisha tendo na mtendaji.

Baada ya kufafanua dhana hizo, tumejadili kwa mapana huku tukitoa mifano anuwai ya ukiushi wa vipashio mbalimbali katika sentensi. Vipashio ambavyo tumeviangazia ni: nomino, vitenzi, vielezi, viunganishi na vihusishi. Tumetoa sababu za ukiushi huo na kutoa maoni yetu vile sentensi hizo zingeandikwa katika hali ya kawaida.

Fauka ya hayo, tumegusia ufupi na urefu wa sentensi katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Tumebainisha kuwa mwandishi amechanganya sentensi fupi fupi na sentensi ndefu ambazo zimedhihirisha mtindo wake wa uandishi. Tumeangazia majukumu na athari ya sentensi fupi na ndefu katika diwani hii.

Isitoshe, tumemulika nafasi ya uakifishi katika sintaksia katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.* Tumeonyesha alama za uakifishi alizotumia mwandishi kwa wingi na kutoa sababu ya kuzitumia pamoja na athari yake katika sentensi.

**Tanbihi**

1. Kategoria za maneno ni dhana inayohusu aina mbalimbali za maneno ambayo hutumika katika muundo wa sentensi. Aina hizo za maneno ni pamoja na: nomino, vitenzi, viwakilishi, vivumishi, vielezi, vihusishi, viunganishi, vihisishi, vionyeshi na vibainishi.

2. Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye mkusanyiko wa maneno yenye kutawaliwa na neno kuu kama kikundi nomino na kikundi tenzi.

3. Kishazi ni dhana inayorejelea fungu la maneno lenye muundo wa kiima na kiarifu lakini ambalo limo ndani ya sentensi kubwa.

4. Massamba D. et al. *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo,Dar es Salaam,* TUKI, 1999, uk. 165.

# SURA YA TATU

## UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA *ARUSI YA BULDOZA*

### 3.0 Utangulizi

Semantiki ni tawi la isimu ambalo hujishughulisha na uchambuzi wa lugha katika kiwango cha maana. Sura hii inashughulikia namna mwandishi amekiuka matumizi ya lugha ya kawaida ili kuleta maana mbalimbali katika kazi yake. Tunajadili matumizi ya methali, semi, tamathali za usemi na mbinu nyingine za lugha kama vile majazi, takriri, tanakali za sauti, mdokezo, kuchanganya ndimi, nidaa, ritifaa na taswira. Mbinu hizi za lugha zinahusiana na semantiki kwa sababu zinabeba maana mbalimbali katika muktadha zinamotumiwa.

### 3.1 Methali

Fasili mbalimbali zimetolewa kuelezea methali. Aghalabu fasili zote zinazotolewa huzingatia kipengele cha kisemantiki na pragmatiki au matumizi[1]. Mbatiah M. (2001:45) anafasili methali kama "kauli fupi iliyosheheni maana na ujumbe, na inayochukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha ukweli na busara." Anafafanua kuwa methali ni sehemu ya turathi za kimapokeo za jamii. Zinabeba falsafa, mila, miko na desturi za jamii.

Mwandishi ametumia methali anuwai katika hadithi fupi zilizomo katika diwani ya *Arusi ya Buldoza* kutegemea muktadha wa mazungumzo ya wahusika. Katika hadithi 'Njia Fupi' (uk. 39) mwandishi anasema kuwa 'tabia ya mwanadamu ni ya uwamba ngoma, kila mmoja anavutia kwake'. Mwandishi ameitumia methali hii kurejelea tabia ya Fumu ya kutaka kujinufaisha kwa kuwa na jicho la nje bila kumfikiria mkewe Naima Mambo.

Tabia ya Fumu ya udanganyifu na ukosefu wa uaminifu katika ndoa inadhihirika wazi. Anajipenda na hajali hali wala hisia za mkewe kuhusu tabia yake ya uzinzi.

Aidha, katika hadithi hii, Naima anapomfumania mumewe Fumu katika nyumba ya Mama Kitimbi, anamwambia kuwa 'njia ya mwongo ni fupi' (uk. 44). Methali hii ina maana kwamba mtu mwenye tabia ya kudanganya huishia kupatikana siku moja kama alivyopatikana Fumu.

Katika hadithi ya 'Baku na Bakuzi', tunaona kuwa maudhui ya unafiki na uwongo wa waganga yanaangaziwa. Maryam mke wa Bakuzi anamwendea mganga Baku akitaka kujua chanzo na tiba ya ugonjwa wake. Baku kwa unafiki na uwongo anamuueleza Maryam kuwa mume wake Bakuzi ndiye anataka kumroga afe ili arithi mali yake. Ndiposa Maryam anamwambia shoga yake Mashavu kuwa 'na kinilacho ki nguoni mwangu' (uk. 69). Kwa kawaida, methali hii huandikwa 'kikulacho kinguoni mwako' kurejelea mhusika wa nafsi ya pili umoja. Lakini methali hii imepinduliwa kimaana na Maryam akijirejelea mwenyewe anaposema 'kinilacho kinguoni mwangu'. Huu ni ukiushi wa maana. Methali hii imetumiwa kumrejelea Bakuzi mumewe Maryam kuwa yeye ndiye anayetaka kumroga afe. Inashadidia ukweli kuwa mtu anayeweza kukudhuru ni yule anayekufahamu yaani rafiki yako au jamaa wa karibu.

Mwandishi ametumia methali 'kiumbe akipenda chongo huita kengeza' (uk 109) katika hadithi 'Mwanaarusi'. Methali hii hutumiwa kumrejelea mtu anayempenda mtu au kitu ambacho kina ila lakini haitambui. Ali anampenda msichana anayeitwa Mwanaarusi.

Msichana huyu anatoka katika familia ya kimaskini lakini Ali hataki kufikiria jambo hilo kwa vile amevutiwa naye na anataka amwoe. Anamkumbusha kuwa pindi tu akikubali kuolewa naye, atampa kila kitu na maisha yake ya kuuza mandazi yatakoma. Hata hivyo, Mwanaarusi anakataa ombi la Ali kwa vile yeye hatamani mali.

Katika hadithi 'Mgonjwa', Hiba anasema kuwa 'Mungu akikupa kilema hukupa na mwendo' (uk. 114). Anajirejelea kuhusu hali yake ya kukatwa mguu alipopata ajali barabarani. Sababu kuu ya kupata ajali hiyo ilikuwa mapenzi yake kwa Dkt. Haji. Kupitia mhusika huyu mwandishi anamaanisha kuwa Mungu amjaliapo mtu kuwa na ulemavu humjalia na mwendo. Hii ina maana kwamba Mungu hawezi kumyima mtu vitu vyote.

Mwandishi ametumia methali kwamba 'kweli sasa imedhihiri na uwongo hauna budi kujitenga' (uk. 141) katika hadithi 'Mwungwana' Methali hii inarejelea hali ya kwamba Bwana Haji amemfumania mke wake Saada na Bwana Haji nyumbani kwake usiku wa manane wakifanya mapenzi. Bwana Haji alipata fununu kuhusu tabia ya mke wake. Alitaka apeleleze ajue ukweli wa dai hilo. Leo ndio amepata ukweli huo. Amesimama nje ya mlango wake akingoja afunguliwe mlango na mke wake Saada. Kwa hivyo methali hii inafumbata hali hiyo vizuri kuwa Saada ni mzinzi na hawezi kumdanganya mumewe tena. Baadaye, Bwana Haji anampa talaka Saada mbele ya wazazi wake.

'Maskini haokoti, akiokota huambiwa keba' (uk. 153) ni methali iliyotumiwa katika hadithi 'Maskini Haokoti'. Mussa ambaye anatoka familia ya kimaskini anampenda msichana aitwaye Halima. Halima anatoka familia tajiri. Othman, rafiki ya Mussa

anamshawishi Halima ampende. Halima anampenda na kumtupa Mussa. Wanapanga arusi ya siri na kumwalika Mussa ahudhurie. Mussa anashangaa kwa tukio hilo. Mussa anajipoza moyo kwa kutumia methali hii inayoafiki kitendo cha rafiki yake Othman kumnyanganya mpenzi wake. Methali hii imetumiwa kuonyesha dharau ya wenye uwezo kuwahusu wanyonge.

## 3.2 Semi

Wamitila K. (2003: 166) anaeleza kuwa semi ni neno lenye upana ambalo hutumiwa kuelezea matamko fulani yanayoelezea ukweli fulani. Aidha, semi ni kauli za maneno kadha yenye maana iliyofichwa.

Said A. Mohamed ametumia semi nyingi katika hadithi tofauti tofauti kuelezea hali fulani zinazowakumba wahusika. Kwa mfano katika 'Arusi ya Buldoza' ametumia usemi 'alikata tamaa!' (uk. 7). Msemo huu unahusu hali ya Mjaka, mhusika mkuu kupoteza matumaini kuhusu kuwepo haki na maendeleo katika nchi yake kwa kuwa watu wachache wanawanyanyasa walio wengi. Aidha, tunaambiwa katika hadithi hii kuwa 'moyo ulimpiga beni'. Msemo huu una maana kuwa moyo wa Mjaka ulimdunda sana kutokana na hofu.

Katika 'Dhuluma Inamojificha' Siti anatumia msemo 'chai ya mkandaa' (uk. 10) wanapozungumza na shoga yake Zaina. Msemo huu una maana ya chai ambayo haina maziwa. Wakati mwingine huitwa chai ya rangi.

Mwandishi pia ametumia semi 'kujenga upenu' (uk. 70) katika hadithi 'Baku na Bakuzi'. Anarejelea kitendo cha Baku aliyejidai kuwa mganga hodari, kumtenganisha Maryam na mume wake Bakuzi ili apate nafasi ya kuwa na uhusiano na Maryam. Msemo huu una maana ya kuishi na mke au mume wa mtu nje ya ndoa baada ya kumfitinisha na mume au mkewe. Hivyo ndivyo alivyonuia kufanya Baku kwa kumdanganya Maryam kuwa Bakuzi anamroga ili adai talaka kutoka kwa mume wake. Hata hivyo, Bakuzi alimzidi Baku maarifa. Hatimaye alimwadhibu viboko ishirini kupitia rafiki yake Bwana Maftaha.

Katika hadithi 'Tofauti' kuna matumizi ya msemo walibaki 'wakipiga domo' (uk. 79). Msemo huu unarejelea vijana ambao wanabarizi kwenye upwa wa bahari wakati wa jioni. Maana yake ni kuwa vijana hao wanazungumza bila ya kuwa na kazi ya kufanya. Aidha katika ukurasa wa 85, mwandishi anasema kuwa Fadhila na Salim walijikuta wamelikalia jabali 'sako kwa bako'. Maana yake ni kuwa walikuwa wamekaa bega kwa bega. Msemo huu unaonyesha namna walivyokaribiana katika kuketi kwao.

Katika 'Uhuru wa Subira' mwandishi anaelezea namna mlango ulivyofunguka baada ya Mrisho kuupiga teke. Anasema kuwa teke moja, mlango wa kumbesa 'ulisalimu amri' (uk. 96). 'Salimu amri' ni msemo unaotoa maana ya namna mlango ulijiachilia ukaanguka kwenda ndani. Mrisho anapoingia ndani ya nyumba, anapata maiti ya mke wake Subira ikining'inia kwenye boriti ya dari. Subira alijiua baada ya kuona kuwa mateso ya mume wake yamezidi. Aidha, babake Mzee Farijala alichangia Subira kujiua kwa vile alimpiga sana akimwambia amnyenyekee mume wake siku zote.

Msemo fukara 'usiye nyuma wala mbele' umetumiwa katika ukurasa wa 125 katika hadithi 'Baba'angu'. Msemo huu umetumiwa na msimulizi wa hadithi 'mimi' akirejelea hali yake ya kutokuwa na uwezo wowote hasa baada ya kufutwa kazi. Hakuwa na pesa zozote za kutumia ndiposa aliandamana na rafiki yake Makame aliyekuwa na shilingi ishirini kwenda kwa Mzee Mtaimbo kunywa pombe aina ya tende ili asahau shida zake.

## 3.3. Tamathali za Usemi

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001:77), tamathali ya usemi ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Kwa hivyo, tamathali ya usemi ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine. Tamathali za usemi zina mchango mkubwa katika kuifanya kazi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa.[2] Mifano ya tamathali za semi ni kama tashbihi, sitiari, tashhisi, tasifida, chuku, tabaini, maswali ya balagha na dhihaka.

### 3.3.1 Tashbihi

Msokile M. (1992: 54) anafafanua kuwa aina hii ya tamathali hutumia mlinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi: "kama", "mfano wa", "mithili ya", "sawa na" na "mfano wa". Mwandishi hutumia ulinganishi huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini.

Katika hadithi 'Dakika ya Mwisho', mwandishi anatueleza namna msichana mtumishi katika mkahawa wa *Lovers Corner* alirudi na chupa na gilasi kumhudumia Yunus. Tunaelezwa:

> Punde alifika tena. Akaja kama kijiko kinavyokorogwa kikombeni. (uk. 57)

Katika dondoo hili, mwandishi anatuchorea picha ya mwendo wa msichana huyo. Inaelekea kwamba msichana huyo alikuwa na mwendo maridadi ambao ulimvutia Yunus alipomkagua kwa macho yake.

Kwa upande mwingine katika hadithi 'Tofauti', Salim anamweleza Fadhila namna alivyompenda msichana aliyeitwa Salha kabla ya kupatwa na ajali iliyosababisha Salha kufariki na Salim kukatwa mguu wake. Salim anasema:

> Tulipendana sana mfano wa roho na kiumbe. (uk. 86)

Kwa kutumia maneno 'mfano wa', Salim anasisitiza mapenzi aliyokuwa nayo kwa mpenzi wake Salha. Msisitizo huo haungejitokeza kama Salim alisema kuwa alimpenda Salha.

Aidha, katika hadithi 'Mkono wa Salama', tunapata mhusika Salama akiwaza namna ameishi na mume wake Simba aliyekuwa katili kwa miaka kumi na tano katika machaka, mahali palipojitenga kabisa na watu wengine. Anashangaa:

> Salama alilochelea siku zote ni binafsi ya maskani yenyewe. Nyumba katikati ya msitu kama aliyeolewa na zimwi!
> (uk. 99)

Kwingineko katika hadithi 'Pigo la Tamaa', tunaelezwa namna Said walivyokutana na msichana kwa jina Salma Masoud hospitalini akavutiwa na urembo wake. Ndiposa mwandishi anamsifu kuwa:

> Said alipoinua uso macho yake yalitua juu ya msichana mfano wa malaika.
> (uk.164)

Mwandishi anafananisha uzuri wa Salma Masoud na Malaika. Lengo lake ni kusisitiza urembo wa msichana huyo.

### 3.3.2 Sitiari

*Encyclopedia Americana* (1977: 1996) juzuu la 11 inaeleza tamathali ya sitiari kwamba ni ulinganisho kati ya vitu viwili tofauti hivi kwamba kimoja kinapewa sifa za kingine. Sitiari hukuza sifa ya ulinganishi kwa kusema kitu fulani ni kingine. Tamathali hii ni muhimu katika kujenga taswira.

Katika hadithi 'Dhuluma Inamojificha' tunakutana na mhusika Siti. Analalamika kuwa mumewe hamtoshelezei mahitaji ya kimsingi kama vile chakula na mavazi

inavyohitajika. Kwa mfano, mumewe Jabu hajamnunulia mavazi ya arusi aliyomwambia miezi mitatu iliyopita. Arusi imekaribia. Kwa hivyo, Siti amenuna na ana hasira nyingi. Amechoka na kutojimudu kwa mumewe kifedha. Kuhusu Siti tunaelezwa:

> Siti alikuwa hana kizuizi tena. Tokea hapo mfereji mbovu, akianza kuboboja hazuiliki!
> (uk. 9)

Siti amelinganishwa na mfereji mbovu. Hivi ni kusema kwamba anaweza kusema maneno yoyote bila kujali. Ndio maana wanazozana na shoga yake Zaina. Isitoshe, anasema kwamba atauza mahaba kwingine apate mtaji ili mumewe adhulumiwe. Mwishowe alisababisha mumewe kuuawa alipojaribu kuiba kwa lengo la kumtimizia mahitaji yake ya arusi.

Maelezo ya umbo la Maryam na urembo wake vimeelezwa na mwandishi katika hadithi "Baku na Bakuzi'. Uzuri wake ndio ulimfanya mganga Baku kumtamani. Maziwa yake yamefananishwa na boribo mbili yaani aina ya matunda fulani. Mwandishi anasema kumhusu Maryam hivi:

> Mashavu ya mfuto, midomo minene, pua ya kusimama, shingo ya muwanzi, kifua kipana chenye kubeba boribo mbili ...
> (uk. 71).

### 3.3.3 Tashhisi

Wales, K. (2001: 349) anafasili tashhisi kuwa "ni tamathali ya usemi ambapo kitu kisicho na uhai, mnyama, kisicho binadamu au chenye sifa za kidhahania kinapewa sifa za binadamu". Tamathali hii imetumiwa na mwandishi kwingi katika hadithi zake ili kuleta mvuto wa kisanaa na athari fulani ya kihisia.

Katika 'Arusi ya Buldoza' tunaelezwa namna kijumba cha Mjaka kimezongwa na vibanda vya majirani wake. Mwandishi anasema:

> Kijumba cha Majaka kimeinamiwa. Tayari kimeshayeyukia vijumba vingine. Tayari <u>kimeshatambaa</u> na kushikana na vibanda vingine vyote.
> (uk. 1)

Kijumba cha Mjaka kimepewa sifa ya ubinadamu. Tunafahamu fika kwamba mtoto mchanga ndiye anayetambaa kabla ya kuanza kutembea. Ikiwa kijumba cha Mjaka kimetambaa, basi kimepewa sifa ya mwanadamu.

Kwingine, katika hadithi 'Riziki Tundu Nyingi' tunaelezwa mazingira ya mji wakati wa asubuhi kunapopambazuka. Maelezo ya hali ya vumbi yanavutia na kunasa nadhari ya msomaji. Tunasoma kuwa:

> Vumbi nalo lilikwisha <u>amka</u> na kushika kasi; kwa hakika <u>halikulala</u>. Kidogo usiku wa manane <u>lilisinzia</u>, lakini punde, katika kiini cha alfajiri baadaye, <u>liligutuka</u> na kushika kani ya kufuatana na kila mtu na kila kitu!
> (uk. 31).

Tunafahamu kwamba haya ni maelezo kuhusu hali ya vumbi mjini wakati wa asubuhi. Mtunzi amekiuka kutumia maelezo kavu kwa kulipa vumbi sifa za mwanadamu za kuamka, kulala, kusinzia na kugutuka.

Katika hadithi 'Mhogo' tunaelezwa namna mheshimiwa anawahimiza wananchi kula mhogo badala ya wali na ngano katika hotuba yake. Baada ya hotuba ya kusisimua anarudi ofisini mwake kufanya kazi. Saa nane mchana, anaenda nyumbani kwake kula chakula cha mchana. Tunaelezwa kuwa mheshimiwa alishangaa alipopata kuwa pamepikwa mhogo kwa vitoweo mbalimbali na mpishi Mzee Sudi. Tunasoma:

> Wote sasa walikuwa wameshakaa juu ya meza na bibiye alifunua kawa, na mhogo ulionona uliwatumbulia macho. (uk.68).

Mhogo umepewa sifa ya kunona na kuangalia kwa macho ukiwa ndani ya kawa kama kwamba una macho.

### 3.3.4 Tasifida

Wamitila K. (2003: 194) anafafanua tasifida kuwa ni matumizi ya maneno ya kupunguza ukali au uzito fulani. Badala ya mhusika kutumia lugha inayoudhi au ya matusi, anatumia lugha inayoficha makali hayo. Aghalabu tasifida hutumiwa baina ya watu ambao hawana budi kuwekeana heshima katika mazungumzo yao.

Tasifida imetumika katika hadithi 'Ukarimu wa Mwihaji'. Tunaelezwa kwamba Mwihaji alimsaidia mheshimiwa wakati gari yake ilipoharibika. Alimwitia fundi akaitengeneza. Aidha, alimpeleka kwake akampatia madafu. Baadaye mheshimiwa alianza kufanya mapenzi na mke wa Mwihaji. Dhuluma hiyo ya mheshimiwa ilipozidi, Mwihaji alipiga ripoti kwa wakubwa lakini hakuna hatua iliyochukuliwa. Mwihaji anatueleza namna alimfumania mheshimiwa kwake nyumbani akifanya mapenzi na mke wake Hadiya. Anasema:

> Na dakika hiyo hiyo nikatoka na mundu wangu kwenda kumhasiri mke wangu... na nilipofika nyumbani nikamkuta hasimu yangu yumo kazini.
> (uk. 25)

Anachomaanisha Mwihaji ni kwamba alipofika nyumbani kwake alimkuta mheshimiwa akifanya mapenzi na mke wake lakini hasemi hivyo wazi kwa kupunguza makali na kuweka heshima fulani.

Katika hadithi 'Usipojua' mwandishi anatufahamisha namna Kibwana alikutana na mamake siku moja asubuhi akienda kazini. Mamake Kibwana alikuwa amelewa na kanga yake ilikuwa imechanikachanika na kuonyesha maziwa yake. Watoto wadogo walikuwa wanamfuata na kumzomea. Tunasoma:

> Ana kanga moja tu kifuani ambayo imechanikachanika na kufedhehi visivyofaa kufedhehiwa.
> (uk.156)

Aidha katika hadithi hii, mamake Kibwana anatumia lugha ya tasifida anapozungumzia Kibwana kuhusu kutofanya mapenzi nje ya ndoa kuwa:

> Na mimi nikijua wewe mwanawe kwani sikumjua mwanamme mwingine.
> (uk. 159)

Mamake Kibwana anasema hivyo kwa sababu anazungumza na mtoto wake. Hana budi kuonyesha heshima kwake.

### 3.3.5 Chuku

Mbatiah M. (2001:6) anasema kwamba chuku ni tamathali ya usemi inayotumia lugha ya kutilia chumvi, aghalabu kwa madhumuni ya kusisitiza. Jambo au hali hukuzwa kupita kiasi. Aidha, mbinu ya chuku hutumiwa kupunguza sifa ya kitu au mtu kwa lengo la kudunisha. Nia ya kuitumia chuku ni kulifanya jambo fulani litokeze kwa uwazi zaidi, kuikuza sifa fulani au kumfikirisha msomaji kwa kuona uzito uliopo.[3]

Katika hadithi ya 'Ukarimu wa Mwihaji', tunaelezwa namna Mwihaji alivyolindwa na askari mahakamani. Tunasoma hivi:

> Lile saa lilipogonga, lilimwamsha Mwihaji kutokana na ndoto hai aliyokuwa akiiota, akajikuta kaketi baina ya askari wawili waliokuwa wanamwangalia hata ule mpweso wake wa macho.
> (uk. 20)

Katika dondoo hili, mtunzi anapiga chuku namna Mwihaji alivyolindwa na askari. Anasisitiza ulinzi mkali wa askari.

Tamathali hii imetumika katika hadithi 'Njia Fupi' ambapo mwandishi anaeleza tabia ya Naima Mambo, mke wa Fumu anavyoweza kufanya mambo ya kushangaza. Tunaelezwa

> Unafanya mchezo nini? Ukisikia Naima mambo ndiye huyu; ana mambo kumshinda hata ibilisi. Anaweza kukigonganisha chuma kwa chuma vikawaka mto na kugeuka jivu.
> (uk. 38)

Katika dondoo hili, uwezo na nguvu za Naima mambo zimetiliwa chumvi. Hata hivyo, Naima Mambo, kupitia mpango wa siri na Mama Kitimbi, alimfumania Fumu akichagua mwanamke wa kufanya mapenzi naye katika ukumbi wa Mama Kitimbi. Fumu aliaibika sana.

Mwandishi pia anatueleza mwendo wa gari la Rukia alipomfuata mumewe Kibwana kwenda Kilimahewa akikusudia kujiua katika hadithi ' Usipojua'. Tunasoma:

> Akili ya Rukia ilifanya kazi harakaharaka. Aliwaongoza wazee wake wawili mpaka garini akatia moto gari na kukanyaga mafuta. Gari haikwenda mbio, iliruka.
> (uk.158).

Sababu ya kusema hivyo ni kwamba anasisitiza mwendo wa kasi wa gari hiyo.

### 3.3.6 Tabaini

Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 209) tabaini ni mbinu ya kiusemi ya kulisisitiza jambo kwa kutumia maneno yanayoelekea kutoonyesha msisitizo huo waziwazi. Aghalabu matumizi ya mbinu hii hutambulishwa na kuwepo kwa 'si'.

Siti katika 'Dhuluma Inamojificha', anamweleza shoga yake Zaina namna anavyopata shida na mume wake Jabu. Anamweleza jinsi mume wake ameshindwa kumnunulia nguo nzuri na vyakula vizuri kwa sababu ana kipato cha chini. Siti anasema:

> Shoga we, mume si pawa na meko tu... na hizo nazo kwani anazitimiza? Chakula chenyewe maruweruwe, <u>si</u>kwambii kivazi tena.
> (uk. 10)

Fadhila anaeleza juu ya Salim katika hadithi 'Tofauti' kuwa:

> Salimu si mgumu tu, ni mzohali pia, kwa hivyo alisimama tanda kabisa bila uso wake kubashiri hisia zozote. <u>Si</u> kicheko <u>si</u> huzuni; labda kawaida tu!
> (uk. 82)

Katika 'Uhuru wa Subira', Subira anateswa na mume wake Mrisho katika ndoa yao. Subira anaona kuwa maisha hayo ni sawa na jela. Subira anapigwa na mume wake hasa anapokuwa amelewa. Hali hii imemfanya Subira kuwa na alama alama mwilini na afya yake kudhoofika. Mwandishi anatukumbusha kuhusu subira hivi:

> Siha yake imepeperushwa na maafa pamoja na masaibu ya kilimwengu. Sikwambii bughudha na nyanyaso za mumewe
> (uk. 90).

### 3.3.7 Maswali ya Balagha

Hii ni tamathali ya kuuliza maswali ambayo hayahitaji majibu. Aghalabu maswali hayo hayahitaji majibu kwa sababu majibu yake yako wazi kwa msikilizaji au msomaji. Ni mbinu moja ya kusisitiza usemi, kumfikirisha msomaji na kumshawishi kuhusu jambo au hali fulani.

Tunaweza kusema kuwa mwandishi Said Ahmed Mohamed ametumia maswali ya balagha kwingi katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Mbinu hii inatuelekeza kusema kuwa huu ni mtindo wake wa kumshawishi na kumfikirisha msomaji. Kwa mfano katika 'Arusi ya Buldoza' tunampata Mjaka akiwa juu ya kilima akipunga upepo na kukumbuka namna alivyoteseka kujenga nyumba yake ili afanye arusi na mpenzi wake Kilua. Sasa imebaki siku moja kabla ya arusi kufanyika. Tunaelezwa:

> Na si umebaki muda mfupi tu? Kama wasemavyo, watu, kenda karibu na kumi.Umemla ng'ombe mzima utashindwaje na mkia?
> (uk. 3).

Katika hadithi 'Baku na Bakuzi' mwandishi anazungumzia furaha ya Bakuzi kwa kuwa na mke mzuri – Maryam. Ndiposa anasema:

> Nani aliyesema kwamba pepo haiko duniani? Mbona Bakuzi pepo ya dunia iko mabegani pake, anaamka na kulala nayo, anakwenda akirudi nayo? (uk. 69).

### 3.3.8 Dhihaka

Kuhusu tamathali hii, Wamitila (2003: 194) anasema kwamba msemaji au mwandishi hutumia usemi unaoficha hisia zake kumhusu mtu au kuihusu hali fulani. Kimsingi, pana kinaya fulani katika maneno yaliyotumiwa. Sababu kuu ya kutumia dhihaka ni kumcheka na kumkera mtu.

Mfano mzuri wa dhihaka unapatikana katika hadithi 'Mwungwana'. Katika hadithi hii, Bwana Haji alipata fununu kuwa mke wake Saada ana jicho la nje na Kibwana. Alifanya mpango wa kumnasa na kisha ampatie talaka bila kumpiga Saada wala Kibwana. Leo saa nane za usiku amewafumania. Bwana Haji anaporudi ghafla kutoka baharini, Saada na Kibwana wanashtuka. Kibwana anataka kutoroka lakini Bwana Haji anamwambia:

> Aaa, rafiki yangu Kibwana, hebu poa. Starehe ulizozifuatia utazikimbiaje? Kama unataka kutoka, basi toka kama ulivyoingia, taratibu, na ukipenda, kipo chumba chengine nitakwenda kujitupa huko... <u>tafadhali endelea kustarehe mgeni wangu.</u>
> (uk. 143).

Bwana Haji ananuia kumcheka na kumkera Kibwana. Uungwana wa Bwana Haji kulingana na anwani ya hadithi hii unaonekana pale ambapo hampigi Saada wala

Kibwana baada ya kuwafumania nyumbani kwake. Baada ya Kibwana kutoka anaendelea kumtimizia Saada mambo yaliyolazimu bila kumwuliza chochote wala kumpiga. Anawaita wazazi wa Saada kisha anampatia talaka mbele yao.

## 3.4 Mbinu Nyingine za Lugha

### 3.4.1 Majazi

Hii ni mbinu ya kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi vitendo na tabia zao.[4] Jina la mhusika linakuwa kielelekezi cha tabia yake. Majazi huhusisha pia majina ya mahali. Mbinu hii humsaidia msomaji kufahamu sifa na tabia ya mhusika kwa urahisi sana. Aidha, inaweza kuweka wazi mtazamo wa mwandishi kuhusu wahusika fulani na hata kutoa mwelekeo wa hadithi nzima.

Katika hadithi 'Njia Fupi' tunawapata wahusika wawili ambao ni Naima Mambo, mke wa Fumu na Mama Kitimbi mwenye nyumba ya ukahaba. Mhusika Naima Mambo amepewa jina hilo ambalo linaafiki tabia yake ya kufanya mambo makubwa na ya kushangaza. Anamtega mumewe Fumu mwenye tabia ya uzinzi na kumfumania kwa Mama Kitimbi. Jina la Mama Kitimbi linadhihirisha kuwa ni mtu wa kufanya mambo yasiyo ya kawaida. Anapanga na Naima Mambo ili Fumu afumaniwe akistarehe na mwanamke.

Kwa upande mwingine katika hadithi 'Mkono wa Salama' tuna wahusika kadhaa wenye majina ya majazi. Kwanza tuna Salama na Simba. Neno 'salama' linamaanisha hali ya

kuweko na amani na utulivu.[5] Salama ni mwenye amani na utulivu ingawa mume wake Simba anamwonea na kumpiga magumi na mateke bure. Hathubutu kupigana na mume wake. Simba naye ni mkali. Tunafahamu kuwa mnyama aitwaye simba ni mkali na anaogopewa na wanyama wengi wa msituni na binadamu kwa jumla. Kwa hivyo, Simba ni mkali kwa mke wake ndiposa baada ya kulewa humpiga mke wake Salama. Hata hivyo, kama anwani ya hadithi inavyosema, Salama anamwokoa Simba siku moja usiku anaposhambuliwa na chatu mtoni. Kwa hivyo Salama anaokoa mumewe, ndoa yao na yeye mwenyewe kwa vile Simba anamwomba Salama amsamehe kwa mabaya yote aliyokuwa akimfanyia.

Katika 'Uhuru wa Subira', mhusika Subira anateswa na mume wake Mrisho. Anavumilia mateso hayo. Hali inapokuwa mbaya Zaidi, Subira hataki kuvumilia tena. Anaona afadhali apate uhuru wake japo kwa njia ya talaka waachane na mume wake. Mwishowe inaposhindikana, Subira anajitia kitanzi nyumbani kwake usiku wa manane kabla mumewe Mrisho hajarudi kutoka ulevini.

Awali tulisema kuwa hata jina la mahali linaweza kuwa la majazi. Katika hadithi 'Baku na Bakuzi', Baku anahukumiwa kupigwa viboko ishirini na mganga Maftaha kwenye jiwe la Mwanahaki. Bakuzi anaamuliwa haki yake dhidi ya Baku anayemfitinisha na mkewe Maryam kwa ramli ya uwongo.

### 3.4.2 Takriri

Takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi ya sanaa kama anavyosema Msokile M. (1992:61). Lengo kuu la mwandishi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo ni kulitilia mkazo jambo linaloelezwa. Kwa mfano katika 'Baku na Bakuzi' mwandishi anasisitiza kitendo cha Baku cha ramli ya uwongo kwa Maryam kwa kusema:

> Hana haya. Hana muhali. Hana imani. (uk. 72)

Pana urudiaji wa neno hana. Hii ni takriri ya neno.

Katika hadithi 'Mgonjwa', pana matumizi ya takriri. Mwandishi anamrejelea mhusika Hiba anavyojirembesha ili kwenda kukutana na mpenzi wake Dkt. Haji. Tunaelezwa:

> Amejisinga. Amejikwatua. Amejiremba. Amejisugua.
> Amejipulizia.
> (uk. 113)

Katika dondoo hili pana takriri ya silabi 'ameji' ya kurejelea mhusika Hiba. Lengo la mwandishi hapa ni kusisitiza kitendo cha kujirembesha.

### 3.4.3 Tanakali za Sauti

Hii ni mbinu ya uigaji wa sauti fulani. Maneno yanayotumiwa huonyesha jinsi sauti fulani inavyosikika. Msingi mkuu wa matumizi ya mbinu hii ni kuhakikisha kuwa hali fulani imeelezwa kwa njia kamilifu. Mbinu hii imetumiwa ili kutueleza namna saa kwenye ukuta iligonga katika hadithi 'Ukarimu wa Mwihaji'. Anasema:

> "Ndo", moja!
> "Ndo", mbili!
> "Ndo," tatu! Liligonga lile saa zee lililokubuhu pale ukutani...
> (uk. 17)

Aidha, katika hadithi 'Mtego" tunaipata sauti ya saa pia ikigonga ukutani, chumbani pa Salamuu hivi:

> Hakuna sauti ila tik tak, tik tak za saa ukutani. Moyo wa Salamuu nao ulikwenda tik tak, tik tak, tik tak – waziwazi kabisa.
> (uk. 45)

Katika hadithi 'Mwungwana', tunaipata sauti ya kugongwa kwa mlango na Bwana Haji nyumbani kwake usiku ambapo amemfumania mke wake Saada na Kibwana wakikumbatiana. Mwandishi anaeleza:

> Saa nane za usiku.
> Ko, ko, ko... "Hodi", sauti nzito ya kiume ilibisha hodi.
> (uk. 138)

### 3.4.4 Mdokezo

Hii ni mbinu ambapo mwandishi anaukatiza usemi fulani na kumwachia msomaji kuumaliza. Aghalabu huwa pana vielekezi vinavyoweza kumsaidia msomaji katika kukamilisha usemi huo. Mdokezo unaweza kutumiwa kuashiria maarifa fulani. Inawezekana pia ukasababishwa na sababu ya tasifida. Mwandishi ametumia mbinu hii sana kiasi kwamba imejitokeza kuwa mtindo wake.

Mfano mzuri wa mbinu ya mdokezo ni huu unaopatikana katika hadithi 'Dhuluma Inamojificha'. Zaina anapotaka kujua ni kwa namna gani Jabu hamtimizii Siti mahitaji yake ya chakula na mavazi, Siti anasema:

> Kitanda usichokilalia bibi....ndiyo maana ukauliza lipi.
>
> (uk. 9)

Katika usemi huu wa Siti, tunaona kuwa ametumia methali ambayo hakuikamilisha lakini kutokana na maarifa ya kiusomi tunajua kwamba methali hiyo ingekamilishwa kuwa kitanda usichokilalia huwajui kunguni wake. Methali hii ina maana kwamba hakuna awezaye kuelewa shida ambayo haijamkumba. Kwa hivyo, Zaina hangeelewa shida zinazomkumba Siti na mumewe Jabu katika ndoa yao.

Katika hadithi 'Ukarimu wa Mwihaji', tunampata Mwihaji akiongea na mheshimiwa ambaye gari yake imeharibika. Mwihaji, anatoka kwake kondeni akiwa na jembe lake na

mundu mkononi. Anaamua kumsaidia mheshimiwa ambaye baadaye hakuonyesha fadhila zozote kwa Mwihaji. Tunasoma:

> Basi waonaje tukenda nyumbani ukapumzike, na mimi nitakwenda kumwita fundi hapo... si mbali, aje aitazame gari yako na kisha...
> (uk. 23).

### 3.4.5 Kuchanganya Ndimi

Katika mbinu hii, mwandishi anatumia lugha mbili au zaidi kwa kuchanganya. Sababu kuu ni kuonyesha tofauti za wahusika kwa matumizi ya lugha. Kwa mfano katika hadithi ya 'Riziki Tundu Nyingi' mtunzi ametumia maneno ya Kiingereza 'Christmas' (uk. 31) and 'bar' (uk. 34). Aidha katika hadithi 'Njia Fupi' pana matumizi ya neno 'time' (uk. 39). Isitoshe, maneno 'wine' (uk. 134) na 'party' (uk. 135) yametumiwa katika hadithi 'Mtoro'.

Mfano mwingine wa mbinu hii unapatikana katika hadithi 'Pigo la Tamaa' Bwana Seif na Bimkubwa wanapozungumza juu ya mtoto wao Said. Wanajadiliana kama wamwache Said amwoe mpenzi wake aliyemchagua, Salma Masoud hata kama ni kiwete. Bwana Seif anataka mtoto wao apewe uhuru wa kuchagua analotaka. Mamake, Bimkubwa anapinga kwa kusema kuwa hivyo ni kuharibu jina la wazee wake. Bwana Seif anasema wamwache Said ajaribu, wembe ukimkata atauwacha mwenyewe (uk. 162). Naye mamake Said anamjibu:

> Wakati huo tena, ha, babu we, yaroro hayo, aaa – itakuwa too late!
> (uk.162)

Tunaweza kusema kuwa Bimkubwa ni msomi kwa vile anachanganya Kiingereza na Kiswahili tukifahamu kwamba maneno hayo ya Kiingereza yana maana aliyokusudia kuitoa kwa Kiswahili kuwa mwanao atapotea na itakuwa vigumu kurekebisha mambo.

Mbali na kuchanganya Kiingereza na Kiswahili, pana matumizi ya Kiarabu na Kiswahili katika hadithi ya 'Baku na Bakuzi'. Baku anatumia maneno ya Kiarabu kumpigia Maryam ramli ya uwongo. Tunasoma:

> Hebu, ngoja kwanza. Labda bao nimelikosea ...*Kamar, mushtar*...Lo *mirhi* amekaa juu...Na wewe jina lako linaanzia *mim* na yeye jina lake linaanzia *bee*. Na baba zenu wanaanzia *sin,* kama si ukorofi huo ni nini basi?
> (uk. 74).

### 3.4.6 Nidaa

Ni mbinu ambayo hutumika kuonyesha hisia fulani kama vile mshangao, furaha, hasira au kukataa jambo fulani. Alama ya mshangao hatumiwa kuleta hisia iliyokusudiwa. Kwa mfano, katika 'Baku na Bakuzi', Mashavu, shoga yake Maryam anashangaa Maryam anapomwambia kuwa alipoenda kwa mganga Baku kupigiwa ramli, aligundua kuwa chanzo cha ugonjwa wake ni mumewe Bakuzi anayemroga. Mashavu anashangaa:

Lo! Dunia! Ama kweli usimwamini hata mama 'ako.

(uk. 70)

### 3.4.7. Ritifaa

Mbatiah M. (2001: 70) anaelezea ritifaa kama mbinu ya kifasihi ambapo mtunzi au msemaji anaongea au kuhutubia mtu au kitu kisichokuwepo. Katika hali hii mtu au vitu vinavyohusika ni vya kufikiriwa tu. Mbinu hii humwezesha msemaji kutoa hisia zake kwa njia ya moja kwa moja. Mbinu hii imetumika katika hadithi 'Pigo la Tamaa'.

Said anapokubaliwa na wazazi wake amwoe mpenzi wake Salma Masoud anaingia ndani ya gari yake kuelekea kwao Salma kumuarifu kuhusu kibali cha wazazi. Anapofika kwao Salma, anapata kuwa Salma alijiua kwa kuchelea kutoolewa na Said kwa vile wazazi wake walimkataza asimwoe kwa kuwa alikuwa kiwete. Kwa kupata pigo kubwa, Said anapiga kelele akisema:

> Salma nimekuja kukujibu kuwa wazee wamekubali.
> Kwa nini hukungojea?
> (uk. 167).

Katika dondoo hili, Said anaongea na Salma Masoud ambaye hayuko kwa sababu tayari amekufa. Hawezi kusikia kilio wala kumjibu Said.

### 3.4.8 Taswira

Taswira ni picha ambazo humjia msomaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi hujengwa kwa maelezo fulani. Aidha hujengwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama tashibiha na sitiari. Sababu moja ya kutumia taswira ni kumfanya msomaji aelewe vile mtu au kitu kinavyoonekana na pia kutoa msisitizo fulani.

Said Ahmed ametumia taswira kadhaa katika diwani ya *Arusi ya Buldoza*. Kwa mfano, katika hadithi 'Dakika ya Mwisho', anatupatia picha ya Malaika, mpenzi wa Yunus kwa njia ya maelezo, na tashbihi. Anaeleza kumhusu ifuatavyo:

> Tazama ngozi yako nyororo mno kama shetani. Mwanadamu hapaswi kuibadilisha ngozi yake kuwa namna hiyo. Hebu tazama rangi yako nyeusi ya maumbile imegeuka shaba na i wazi mpaka damu yako inaonekana ikienda ndani. Tazama nywele zako tambi si tambi, nywele za chuma sizo, zinang'ara mng'aro wa ajabu. Mzungu si Mzungu, Mwarabu si Mwarabu, Baniani si Baniani. Mtu mwenye pua iliyofyeteka hapendezi kuwa na nywele za aina hiyo.
> (uk. 60)

Maelezo haya yote kumhusu Yunus yanajenga picha ya sura yake baada ya kutumia vipodozi vingi.

## 3.5 Hitimisho

Katika sura hii, tumeeleza kuhusu matumizi ya lugha katika kiwango cha kisemantiki. Tumeangazia matumizi ya methali na semi mbalimbali na kutoa mifano anuwai kutoka hadithi mbalimbali ili kuthibitisha hoja zetu.

Aidha, tumeangalia namna tamathali za semi zimetumiwa ili kutoa mvuto wa kisanaa, kuonyesha ukomavu wake wa lugha mbali na kupitisha ujumbe wake kwa njia inayoeleweka. Baadhi ya tamathali za usemi ambazo tumezigusia ni pamoja na tashbihi, sitiari, tashhisi, tasifida, chuku, tabaini, maswali ya balagha na dhihaka. Tamathali hizi zina majukumu kadhaa. Zimetumiwa kufafanua maana, kutoa mifano mwafaka, kuibua hisia, kuhuisha, kuchekesha au kurembesha. Muhimu zaidi ni kwamba zina jukumu la kuongeza ujumi katika hadithi zinamotumika.

Mbali na hayo, tumejadili kuhusu mbinu nyingine za lugha ambazo mwandishi amezitumia. Mbinu hizo ni: majazi, takriri, tanakali za sauti, mdokezo, kuchanganya ndimi, nidaa, ritifaa na taswira. Matumizi ya mbinu hizi katika diwani hii yameifanya kuwa na mvuto wa kiujumi, kumburudisha msomaji na kumwondolea ukinaifu wa lugha chapwa.

## Tanbihi

1. Wamitila K. *Kamusi ya Methali*, Longhorn Publishers, 2001, uk. ix.

2. Wamitila K. *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi,* Focus Books, 2003, uk. 193.

3. Kama namba 2, uk. 194.

4. Wamitila K. *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia,* Focus Books, 2003, uk. 106.

5. TUKI, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* (Toleo la Pili) OUP, 2004, uk. 357.

# SURA YA NNE

## MATUMIZI YA MSAMIATI KATIKA *ARUSI YA BULDOZA*

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia uteuzi na matumizi ya maneno katika diwani ya *Arusi ya Buldoza.* Uteuzi unahitaji mwandishi ajiulize ni wapi atumie neno lipi ili kuleta athari anayotaka. Kimsingi, uteuzi huchangia mtindo wa mwandishi katika kazi inayohusika kwa kuwa katika sura ya kwanza tulisema kuwa mtindo ni uteuzi wa namna ya kusema jambo.

Msamiati unafungamana na matukio, muktadha na mazingira ya hadithi fupi. Kwa mfano hadithi inayozungumzia biashara huwa na msamiati unaohusiana na eneo hilo. Msamiati mwingi uliotumiwa na msanii katika diwani ya *Arusi ya Buldoza* umeelezwa katika sehemu ya sherehe. Kwa muhtasari, tunachanganua matumizi ya maneno ambayo si ya Kiswahili Sanifu, maneno ambayo yametoholewa bila kuwa na sababu maalum, matumizi ya maneno kisitiari kwenye vichwa vya hadithi na mageuzo ya maumbo ya maneno na kutumia maneno katika muktadha ambapo hayapaswi kutumiwa.

### 4.1 Msamiati wa Lahaja ya Kipemba

Katika baadhi ya hadithi, mwandishi ametumia msamiati wa lahaja ya Kipemba. Lahaja ya Kipemba ni mojawapo ya lahaja zinazopatikana katika visiwa vya Zanzibar. Kwa mfano, katika hadithi 'Uhuru wa Subira' tunafahamishwa kuwa Mrisho alienda kunywa

pombe akarudi kwake saa kumi na nusu alfajiri huku amelewa sana. Pana matumizi ya maneno ya visiwani kusisitiza kulewa alikolewa Mrisho. Tunasoma:

> Mrisho alirejea kwake kiasi cha saa kumi na nusu alfajiri, na kama kawaida alikuwa *chaa!* Au *chordo,* walichoona watu.
> (uk. 95)

Maneno 'chaa!' na 'Chordo' si ya Kiswahili Sanifu kwa vile hayapatikani katika kamusi ya Kiswahili Sanifu. Ingawa maneno haya yametumika kutilia mkazo kulewa kwa Mrisho, yanaonyesha ukiushi wa mwandishi kutotumia maneno ya Kiswahili Sanifu kama vile 'kulewa chakari' ili kutilia mkazo kulewa kwenyewe.

Katika hadithi 'Njia Fupi', msanii anatusawiria picha ya umbo la Naima Mambo. Fumu ambaye anamtazama mke wake akijipodoa, anamtazama kwa jicho la kumtamani. Tunaelezwa kuwa "mtutumko wa mwili umedhihiri, kumfanya Fumu wakati huu maji aite *mma*" (uk. 41). Neno 'mma' ni msamiati wa visiwani unaorejelea maji kama wasemavyo watoto wadogo. Anachomaanisha mwandishi ni kwamba umbo la Naima Mambo lilimfanya mumewe Fumu kukosa maneno ya kusema.

Katika hadithi 'Baba'angu' msimulizi 'mimi' anashangaa kumwona rafiki yake Makame akinunua pombe kali aina ya tende; nusu chupa yake (Makame) na nusu chupa nyingine ya 'mimi'. Tunasoma:

> Lo! Nilihofu! Nusu chupa. Tena
> ulevi wenyewe *tende!* au chambacho
> wenzetu wa Dar, gongo!
> (uk. 125)

Neno 'tende' lina maana ya pombe unaotengenezwa kwa tende huko Pemba. Unafanana na ulevi wa gongo.

## 4.2 Msamiati wa Utohozi

'Kutohoa' ni kuchukua neno kutoka lugha fulani na kulifanyia mabadiliko fulani ili lichukue sura na matumizi ya lugha pokezi.

Mwandishi ametohoa baadhi ya maneno kutoka lugha ya Kiingereza bila kuwa na sababu maalum ya kufanya hivyo. Huo ni ukiushi. Kwa mfano katika hadithi 'Dhuluma Inamojificha', Siti anamwambia shoga yake Zaina kuwa:

> Na Jabu nilimwambia zamani kwamba kesho nakwenda arusini, khanga sampuli mpya ya kisutu na kanzu *redimedi* na viatu bulbul vya kisasa vya mchomeko na mchuchumio. (uk. 10)

Neno 'redimedi' limetoholewa kutoka kwa maneno ya Kiingereza 'ready made' yenye maana ya kitu ambacho tayari kimetengenezwa kwa matumizi fulani. Hivyo basi ' kanzu redimedi' ina maana ya kanzu ambayo tayari imeshonwa ili kuuzwa. Mwandishi hana sababu maalum ya kutumia neno 'redimedi' kwa sababu katika lugha ya Kiswahili tuna msamiati wa 'nguo ya kutungua' ambao unarejelea nguo iliyoshonwa tayari kwa kuuzwa.

Mbali na utohozi unaohusu kukopa neno kutoka lugha moja na kulifanyia mabadiliko katika lugha pokezi, pana mtindo wa msanii kuchukua maneno ya lugha ya Kiingereza

kama yalivyo na kuyatumia katika hadithi zake. Aghalabu maneno haya yamewekwa katika alama za nukuu kuonyesha kuwa maneno hayo si ya Kiswahili.

Katika hadithi 'Riziki Tundu Nyingi' tunapata namna wauzaji wa magazeti wanaimba nyimbo za matangazo ya magezeti ili kuwashawishi wateja wanunue. Tunaelezwa:

> Wauza magazeti, wakubwa kwa wadogo,walikuwa wameshaenea kila kipembe, huku wakirukaruka na kutua na huku wakiimba nyimbo za matangazo... "Habari motomoto... Christmas inasonga ...Nunua *Mkombozi,* nunua *Hot News* nunua *The Worker,* nunu..."wote walikuwa katika hamkani.
> (uk. 31).

Neno 'Christmas' limetumika pale ambapo neno 'Krismasi' la Kiswahili Sanifu lingetumika badala yake. Maneno ya Kiingereza yaliyoandikwa kwa herufi za mlazo ni anwani za magazeti yanayouzwa ili watu wasome.

Katika hadithi 'Njia Fupi' Naima Mambo anajikwatua kabla ya kwenda kwa Mama Kitimbi ambapo amepanga kumnasa mume wake Fumu katika tabia yake ya uzinzi. Tunasoma:

> Mipango kaipanga mwenyewe. Hakuna sababu asiitekelezea mwenyewe na kuona taathira yake mwenyewe. Naam hakujali. Aliazimia kuchukua 'time' yake, huku kanuwia taathira kuikuza na ikibidi kuitia shadda na mada, kwa makusudi ya kumwona simba anayemtega kaingia mtegoni na kusononeka.
> (uk. 39)

Hapa neno "time" limetumika badala ya neno "wakati" la Kiswahili Sanifu ili kuonyesha namna Naima Mambo hakuwa na haraka yoyote katika mipango ya kumtega mumewe ili atakapopatikana aaibike na kuacha tabia yake ya uzinzi.

Katika hadithi 'Tofauti' tunampata msichana kwa jina Fadhila akimngoja kijana Salimu fuoni wakati wa magharibi ili amwelezee mapenzi yake kwake. Tunaambiwa kuwa watu wengi walikwisha ondoka ufuoni hali ikatulia ila 'waliobaki ni vijana wachache wa kiume wanaojiita *mabrother-men* (uk. 79). Neno hili limetumiwa kwa utani kuonyesha uhuni wa vijana hao wa kiume kwa vile walikuwa na shauku ya siri ya kukipenda kiza.

Kwingineko, katika hadithi 'Mtoro' tunampata Mwatima, msichana anayetoka kijijini na Kipepe anayetoka mjini wakizungumza. Kipepe anamkaribisha Mwatima achague kinywaji kati ya vinywaji alivyokuwa navyo kwa kumwuliza 'Utakunywa nini 'wine', soda au bia?" (uk.134). Tafsiri ya neno 'wine' katika Kiswahili ni mvinyo. Matumizi ya neno hilo yanadhihirisha kwamba Kipepe ni mweledi wa vinywaji kuliko Mwatima ambaye anatoka kijijini.

Kipepe anapomchukua Mwatima hadi mjini, anakutana na wasichana wenzake Masika, Bihija na Shukrani wamejipamba tayari kwenda klabu usiku kunywa na kucheza densi. Wanamwuliza:

> He! Za wapi?
> Umekwenda kukaa shamba huko mpaka
> Saa mbili, umesahau kuwa leo kuna
> 'party' ya Ruzuna...
> (uk. 135)

Neno 'party' limetumika kwa maana ya karamu au hafla ya Ruzuna. Katika sherehe hiyo kulikuwa na wasichana na wanaume waliokunywa pombe na kucheza densi wawiliwawili. Tabia hiyo ilikuwa ngeni kwa Mwatima. Hatimaye, Mwatima anaamua kurudi nyumbani aendelee kuishi na nyanyake kuliko kuonja maisha ya uovu ya mjini.

## 4.3 Msamiati wa Kisitiari Katika Vichwa vya Hadithi

Kwa majibu wa Wamitila K. (2003: 202) sitiari ni "tamathali ya usemi ielezeayo sifa za kitu fulani kwa kusema kuwa ni kingine." Msanii ametumia msamiati wenye maana fiche katika baadhi ya vichwa vya hadithi zake. Kwa mfano hadithi 'Arusi ya Buldoza' ina neno buldoza kama sitiari.

Neno 'buldoza' limetoholewa kutokana na neno la Kiingereza 'bulldozer'. Lina maana ya tingatinga yenye nguvu nyingi za kulima barabara na kubomoa majengo makubwa. Katika hadithi hii, 'buldoza 'inasimamia nguvu au mamlaka ya serikali. Serikali kupitia kwa askari inatumia rungu, bunduki na farasi kupiga wananchi akiwemo Mjaka eti kwa sababu wanaunga mkono chama cha haki. Wananchi hawana uwezo wa kupigana na serikali kwa sababu ni wanyonge. Arusi ya Mjaka na Kilua haifanyiki kwa kuwa nyumba ilibomolewa. Neno 'arusi' pia linaweza kusimamia mipango ya wananchi kujiunga na chama cha haki. Mpango huo unatibuliwa na serikali kama arusi ya Mjaka ilivyotibuka.

Neno 'dhuluma' katika hadithi 'dhuluma Inamojificha' limetumika kistiari. Siti,anafikiria kuwa dhuluma inapatikana katika kufanya mapenzi nje ya ndoa ili mumewe Jabu

alaumiwe. Anataka kufanya mapenzi nje ya ndoa ili apate pesa za kujinunulia mavazi ya arusi ikiwa mumewe hawezi kumnunulia.

Jabu, mumewe Siti, anafanya juhudi kupata pesa za kumnunulia mavazi ya arusi. Anaposhindwa kupata pesa, anajaribu kumwibia mwanamke mmoja mkoba wake akikusudia kuwa humo mkobani atapata pesa. Lakini anashikwa na kupigwa hadi kufa na umma wenye hasira. Tunaambiwa kuwa:

> Siti na Shoga'ake Zaina walifika hospitali kuchukua maiti wao. Siti alilia sana na kujuta. Zaina alimnyamaza na kumkumbusha, "Ndani ya dude linaloitwa 'fedha' ndimo dhuluma inamojificha.
> (uk. 16)

Tunaona kwamba tofauti na alivyoamini Siti kuwa dhuluma inapatikana kwa kufanya mahaba nje ya ndoa, kwa hakika dhuluma inajificha ndani ya pesa. Kwa hivyo, pesa ndiyo sitiari ya dhuluma kulingana na anwani ya hadithi. Pesa ndizo chanzo cha dhuluma au uovu katika jamii.

Katika hadithi 'Riziki Tundu Nyingi' tunaona namna watu tofauti tofauti wanavyopata riziki zao. Riziki ni kitu kinachopatikana kutokana na kazi na humwezesha binadamu kuishi. Namna watu tofauti wanavyotumia mbinu tofauti kujipatia riziki zao katika hadithi hii inafananishwa na namna tundu zilivyo nyingi.Kuna njia nyingi za watu kujipatia riziki katika hadithi 'Riziki Tundu Nyingi'.

Kwa mfano katika hadithi hii, tunaambiwa kupitia mhusika Sururu kuwa kuna mtu anayeketi chini ya pipa la taka anayekusanya maembe mabovu na kuyala. Aidha, kuna mwanamke kibutu mwenye mtoto anayeomba wapita njia kumsaidia mtoto wake angalau apate chakula. Vilevile kuna mtoto mdogo anayenyatia kuchukua mkate wa kusukuma miongoni mwa vyakula kadha juu ya meza kubwa katika mkahawa. Mbali na hao, kuna pia vipofu wawili mmoja mwanamume na mwingine mwanamke wanaoimba kwa kutumia gitaa na cherewa ili kuwashawishi watu wawapatie pesa za chakula. Kwa hivyo, riziki ni tundu nyingi kwa vipofu, viwete na watu wazima.

Katika hadithi 'Uhuru wa Subira', neno 'uhuru' limetumika kistiari pia. Katika hadithi hii, mwanamke kwa jina Subira anapinga dhuluma na nyanyaso za mumewe Mrisho. Mumewe anapolewa humpiga na kumwumiza. Anataka awe huru kutokana na ndoa ya mateso japo kupitia kwa talaka. Anapoenda kwa babake kushtakia hali yake akitarajia msaada wake, babake naye anampiga na kumwambia amnyenyekee mumewe.

Juhudi zake za kudai uhuru zinapogonga mwamba, Subira anarudi kwa mumewe. Usiku wa manane kabla ya mumewe kurudi kutoka ulevini, anajitia kitanzi. Kwa kukosa uhuru aliotaka, anaona kuwa uhuru unaweza kupatikana kupitia kwa kifo.

## 4.4 Ukiushi Katika Maumbo ya Maneno

Umbo ni sura ya kitu kinavyoonekana. Maneno mengi yameandikwa kwa mtindo wa mlazo. Sababu moja ya kuyaandika kwa mlazo ni kuyafanya yaonekane wazi tofauti na

maneno yaliyoandikwa kwa mtindo wa wima. Si waandishi wengi wanaoandika hivyo. Huo ni mtindo wake wa kukiuka mazoea ya uandishi.

Mbali na kuandika maneno mengi kwa mlazo, msanii ametumia herufi nzito katika baadhi ya maneno na hivyo kubadilisha sura za maneno hayo. Maneno hayo yanaonekana kwa urahisi kuliko yale yaliyoandikwa kwa mtindo wa kawaida. Sababu ya kimsingi inayomfanya kutumia herufi nzito ni kutoa msisitizo.

Baadhi ya maneno yaliyoandikwa kwa herufi nzito ni kama: **'usinifuatefuate'** (uk. 51) katika hadithi 'Mtego', **'kwa ghibu'**(uk. 81), katika hadithi 'Tofauti' **kindumbwendumbwe'** (uk. 107) katika hadithi 'Mwanaarusi' na **'niburai'** (uk. 145) katika hadithi 'Maskini Haokoti'.

## 4.5 Ukiushi katika Ngeli za Maneno

Ngeli ni kundi la nomino lenye sifa zinazofanana kisarufi katika baadhi ya lugha. Katika hadithi 'Mhogo', tunashuhudia ukiushi katika ngeli. Tunasoma kuwa "Ilipofika kiasi cha saa tano hivi, <u>mtu</u> alikuwa kajaa uwanja wote wa Mwembe-tondoo hata ikawa pa kutema mate hapana" (Uk. 63). Nomino 'mtu' inapatikana katika ngeli ya kwanza ilhali nomino 'watu' inapatikana katika ngeli ya pili. Mtunzi anapotumia nomino 'mtu' katika ngeli ya kwanza kurejelea wingi wa watu badala ya kutumia nomino 'watu' walikuwa wamejaa uwanja wote ni mtindo wake wa kutumia maneno kwa ukiushi kueleza wingi wa watu kwa njia isiyozoeleka.

### 4.6 Msamiati wa Sajili

Pana matumizi ya maneno katika hadithi kutegemea mahali tukio linavyotokea. Lugha inaoana na shughuli ya mahali penyewe. Kwa mfano, Baku katika hadithi 'Baku na Bakuzi' ni mganga mjanja ambaye anatumia maneno ya Kiarabu kupigia Maryam ramli.Tunasoma:

> Hebu, ngoja kwanza. Labda bao nimelikosea ...*Kamar, mushtar* ...Lo *mirhi* amekaa juu ...Na wewe jina lako linaanzia *mim* na yeye jina lake linaanzia *bee.* Na baba zenu wanaanzia *sin,* kama si ukorofi huo ni nini basi? Rafiki adui, mpenzi adui, toka llini? Ndio leo. Baku alisema na bao lake bila kumtazama Maryam.
> (uk. 74-75)

Maneno hayo ya Kiarabu yanaonyesha lugha ya vitisho na isiyoeleweka wanayoitumia waganga kuwafanya wateja wao waamini ukweli wa uganga wao.

Katika hadithi 'Mkono wa Salama' tunapata lugha inayotumiwa kwa Hamisi Kirobo katika uuzaji na ununuzi wa pombe. Simba, mume wa salama anapitia huko kunywa kabla ya kwenda kumpiga mke wake kama mazoea yake. Anakuta watu wengi huko. Tunasoma:

> Wakati huu, Sariboko ndiye aliyekuwa nahodha wa jahazi.
> "Nibu," anapima. "Robo," anatia. "Nusu," anatoa.
> "Mzinga, " anamimina.
> (uk. 102).

Maneno yote yaliyowekewa alama za nukuu ni msamiati wa kutaja vipimo mbalimbali vya pombe kwa Hamisi Kirobo. Kwa mtu asiyeelewa wala kunywa pombe kwa Hamisi Kirobo hawezi kuelewa vipimo hivyo. Maneno hayo yamewekewa alama za kunukuu kuonyesha kwamba ingawa ni ya Kiswahili Sanifu, yametumiwa kwa namna isiyo ya kawaida kutegemea mahali penyewe.

Hadithi 'Ukarimu wa Mwihaji' ina mifano mingi ya matumizi ya msamiati wa mahakama. Baada ya hakimu Maisha kutoa hukumu isiyo ya haki kwa Mwihaji, wakili mmoja anasimama akitaka kesi ianzishwe upya ili amtetee Mwihaji. Tunasoma:

> Mimi ni mwanasheria mheshimiwa hakimu...kwa mujibu wa kesi ilivyokwenda, naona mshtakiwa hajatendewa haki, najitolea kesi hii niisimamie mimi kumuhami mshtakiwa, naomba ianzishwe tena.
> (uk. 27).

Lugha hii ni sajili[1] ya sheria. Sajili ya sheria husikika kwa wingi mahakamani. Kwa mujibu wa Buliba A. na wenzake (2006:51) "msamiati unaotumika katika sajili hii unalenga kuwakilisha mifumo ya maana zinazofasili nguzo za haki na kuwajibika kwa watu kama raia au wageni wa nchi." Katika dondoo hili, kuna matumizi ya maneno ambayo aghalabu hutumika mahakamani. Mifano ya maneno hayo ni kama: 'mwanasheria', 'mheshimiwa hakimu', 'kesi', 'mshtakiwa' na 'haki'. Hali kadhalika, sajili ya sheria kwa kawaida hutumia sentensi ndefu kupita kiasi. Sababu kuu ni kutaka kutoa ufafanuzi usio na utata wowote.

## 4.7 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangazia msamiati wa mwandishi katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Tumeona namna msanii ametumia msamiati kwa upekee fulani. Ana uhuru mkubwa wa kutumia msamiati kwa ukiushi fulani ili kupitisha ujumbe kwa msomaji. Uhuru wa kuteua msamiati wa kutumia haumfungi sana kuzingatia sarufi ili kueleza mawazo na hisia zake. Jambo hili linachangia katika upekee wake wa mtindo katika diwani hii.

## Tanbihi

Ni dhana inayorejelea matumizi ya lugha kutegemea muktadha.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunawasilisha hitimisho la utafiti wetu. Sura hii ina sehemu zinazoshughulikia matokeo ya utafiti huu, umuhimu wa utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi juu ya diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*.

### 5.1 Muhtasari wa Matokeo

Katika utafiti huu, tumechunguza mtindo katika hadithi fupi za diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Katika uchunguzi wetu, tumeangazia mtindo katika viwango vitatu ambavyo ni: sintaksia, semantiki na msamiati. Uchunguzi huu umegundua kwamba Saidi Ahmed Mohamed ametumia lugha kwa upekee fulani katika hadithi zake ili kujadili masuala mbalimbali yanayomkumba mwanadamu katika jamii pana. Masuala hayo ni pamoja na siasa, mapenzi, unafiki, matatizo ya asasi ya ndoa na ulevi.

Kuhusu mtindo wa msanii huyu, tumegundua kwamba ametumia ukiushi wa aina mbalimbali kuelezea mawazo yake katika viwango vyote tulivyovishughulikia katika utafiti huu. Kuhusu kiwango cha sintaksia tumebainisha namna mwandishi ametumia ukiushi kupanga upya kategoria za maneno katika sentensi. Tumeona kuwa sababu kuu ya ukiushi huo ni kutilia mkazo kitendo, hali au wazo fulani katika hadithi zake. Vilevile,

tumegundua kwamba sentensi fupi na ndefu zimechangia katika mtindo wake wa kujieleza. Isitoshe, namna alivyoakifisha kazi yake imeonyesha upekee fulani kimtindo.

Aidha, katika kiwango cha semantiki, tumeona kwamba kuna ukiushi wa kimaana kwa kutumia methali, semi na tamathali za usemi ili kuzua maana mbalimbali. Licha ya hayo, tumegundua kwamba methali, semi na tamathali za usemi zimechangia thamani ya kiujumi katika hadithi zilizomo katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.*

Tumebainisha kuwa tamathali za usemi zina umuhimu mkubwa kwa vile zimetumiwa kufafanua maana, kutoa mifano mwafaka, kuibua hisia, kuzua ucheshi mbali na kuongeza ujumi wa kisanaa. Kwa hivyo nadharia tete yetu ya kwanza iliyosema kwamba kuna ukiushi wa kimtindo katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* ni ya kweli.

Katika kiwango cha msamiati, tumegundua kwamba mwandishi amekuwa na uhuru wa kuchagua maneno ya kutumia kusudi awasilishe wazo lake na kuacha athari aliyonuia. Uhuru wa kuchagua msamiati bila kujifunga katika sarufi umechangia sana katika mtindo wake wa ukiushi. Tumebaini kuwa mwandishi ametumia msamiati unaofungamana na matukio, muktadha na mazingira ya hadithi fupi inayohusika. Kwa hivyo, nadharia tete yetu ya pili iliyosema kuwa ukiushi katika mtindo unategemea uteuzi wa namna ya kutumia lugha pia ni ya kweli.

Kwa jumla, Said Ahmed Mohamed ametumia lugha kwa mtindo wa ukiushi. Ameifinyanga lugha yake kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubuni tamathali za

usemi na ukiushi wa kaida za kisarufi. Hakuna waandishi wawili wanaoweza kueleza jambo au suala moja kwa njia sawa. Inategemea elimu, tajriba, uteuzi wa msamiati na lengo la mwandishi mwenyewe.

Nadharia ya elimi-mitindo imetufaa sana katika kuhakiki mtindo katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* kwa kuwa inahusu uchunguzi na uchanganuzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio na masuala katika kazi ya fasihi. Inahusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi fulani na zinazomtambulisha mwandishi anayehusika.

Kuhusu umuhimu wa utafiti wetu, tumethibitisha kwamba mtindo katika utanzu wa hadithi fupi haujashughulikiwa ikilinganishwa na tanzu zingine za fasihi andishi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu, utanzu huu umepuuzwa. Hivyo basi, utafiti huu utatoa mwanga wa kuhakiki mtindo katika utanzu huu kwa vile watafiti wa baadaye watakuwa wanarejelea mchango wa kazi hii kimtindo.

## 5.2 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Katika utafiti huu, tumejikita katika kipengele kimoja cha fani ambacho ni mtindo. Kuna vipengele vingine vya fani kama vile muundo, wahusika na mandhari. Kwa hivyo, kuna haja ya kutafiti juu ya vipengele hivyo na kuonyesha ufaafu wake katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.*

# MAREJELEO


American, Corporation (1977) *Encyclopedia Americana* (Volume 11). New York: American Corporation.

Buliba A. et al. (2006) *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Habwe, J. na Karanja, P. (2005) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Indangasi, H. (1988) *Stylistics.* Nairobi: Nairobi University Press.

Kibera, V. (mh.) (1988) *An Anthology of East African Short Stories.* Harlow: Longman Group Ltd.

Kitsao, J. (1975) "A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts." Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Leech, G. na Short, M. (1981) *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose.* New York: Longman Group Ltd.

Massamba D. et al. (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbatiah, M. (Mh.) (2000) *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mbuthia, E. (2005) "A Stylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories". Tasnifu ya Ph.D (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

McOnyango, O. (Mh.) (2006) *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Mohamed S. A. (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi.* Nairobi: E.A.E.P.

______________ (2002) *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

______________ (2005) *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longman Publishers Ltd.

______________ (2005) *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohochi, E. (1995) "Fani Katika Hadithi Fupi za Kiswahili". Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton.

Msokile, M. ( 1992) *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mwanzi, H. (1995) "The Style of the Short Story in Kenya: An Analysis of the Short Stories of Ngugi wa Thiong'o, Leonard Kibera and Grace Ogot." Tasnifu ya Ph.D. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la pili). Nairobi: Oxford University Press.

Wales, K. (2001) *A Dictionary of stylistics* (2nd Edition). England: Pearson Education Ltd.

Wamitila, K. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

______________ (2003) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Books.

______________ (2001) *Kamusi ya Methali.* Nairobi: Longhorn Publishers.

______________ (1999) *Kamusi ya Misemo na Nahau.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. (Mh.) (2004) *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.